SUPA JACKPOT
TZS. 1,157,290,273
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Jumatano Septemba 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581446
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 3
**TAMISEMI** yamaliza utata mwanafunzi feki kidato V



UKURASA WA 4
**Wachimbaji** wadogo wasifu mpango wa BoT kununua dhahabu



UKURASA WA 4
**UNFPA**, Uingereza zasaidia bil. 23.8/- uzazi wa mpango



# Miezi sita kuamua hatima bosi mpya ndani ya TANESCO

• **Rais** Samia aanika sababu Chande kuondolewa TTCL kwenda Posta... *Endelea ukurasa 2*



Mkurugenzi Mtendaji TANESCO, Gissima Nyamohanga



Posta Masta Mkuu, Maharage Chande

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**JELA MIEZI SITA KUMJERUHI MWANAWE KWA FYEKEO**
MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Singida, imemhukumu Yahya Sungi, Mkazi wa Kitongoji cha Munyu, Kijiji...


UKURASA WA 8
**'WOSIA MWAROBAINI MIGOGORO KIFAMILIA'**
WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umesisitiza Watanzania kujenga tabia ya kuandika wosia kwa kuwa...

## Wanafunzi 460 watumia matundu 6 chakavu ya vyoo
UKURASA 8



# Mwanafunzi ajeruhi mwalimu kwa panga kisa kunyoa ndevu
UK.2

MICHEZO GAMONDI KUISHANGAZA AL MERRIKH UK.24
KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Gerson Msigwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Miezi sita kuamua hatima bosi mpya wa TANESCO

**Jenifer Gilla na Salama Ringo (DSJ)**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameweka hadharani uamuzi wake wa kumhamisha aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande kutoka Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kwenda kuwa Posta Masta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania (TTCL).

Maharage aliondolewa TANESCO Septemba 23 mwaka huu akapelekwa TTCL, lakini juzi usiku aliondolewa huko na kupelekwa kuwa Posta Masta Mkuu, ikiwa ni siku tatu tangu kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

Kiongozi huyo baada ya kuteuliwa katika nyadhifa mpya, aliripoti kazini siku hiyohiyo, lakini aliondolewa jioni yake. Alipokewa ofisini na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

"Kipekee kabisa nikukaribishe ndugu yangu, kaka yangu, rafiki yangu Maharage Chande, karibu rasmi kwenye familia ya wana mawasiliano, Ninajua umetokea huku, ni mshale umerudi nyumbani. Ninamshukuru Rais kwa uteuzi wako, karibu sana!" alisema Nape.

Jana, Rais Samia, akiwaapisha viongozi aliowateua hivi karibuni, alitaja sababu ya kumwondoa Maharage TTCL. Aligundua ana biashara katika kampuni hiyo, hivyo kuwa na maslahi binafsi.

"Na kwa sababu kampuni ile inafanya vizuri, na ndio maana imemwezesha kijana yule kufanya vizuri, nikasema hapana! Usiende mahali ambako una biashara, itakuwa ni mgongano wa maslahi," alifafanua Rais Samia.

Alimwelekeza Maharage kuendeleza kazi iliyoachwa na mtangulizi wake, ili kuliletea maendeleo shirika hasa ya kidigitali.

**BOSI TANESCO**

Rais Samia alitoa miezi sita kwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa TANESCO, Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga, kumaliza changamoto ya kukatika kwa umeme nchini.

Mkuu wa Nchi alimwelekeza mkurugenzi mpya TANESCO kuongeza ufanisi alipoishia mtangulizi wake ikiwamo kufanyia marekebisho ya mitambo ya kuzalishia umeme ambayo haikufanyiwa kwa muda mrefu ili kuondoa kelele za kukatika kwa umeme kutoka kwa wananchi.

"Lakini baada ya hiyo miezi sita nisisikie kelele za kukatika kwa umeme. Kwahiyo, tutasaidiana lakini nenda, ninajua utaweza," alielekeza Rais.

Alisema tatizo la mgawo wa umeme si la mtu mmoja, bali la kitaifa na linasababishwa na mambo mbalimbali, ikiwamo kupungua maji kutokana na ukame unaochochewa na mabadiliko ya tabianchi.

"Maana yake mtu mwingine anaweza kusema Maharage kaondolewa kwa sababu ya kukatika kwa umeme, hapana! Mitambo ile kwa muda mrefu haikufanyiwa matengenezo," alifafanua.

Aliwaelekeza mabalozi wapya John Ulanga na Saidi Yakubu kumsaidia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba kukijenga kitengo cha diplomasia ya uchumi ili kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta hiyo.

"Tupo katika kutengeneza sera yetu ya mambo ya nje, imefika mbali lakini ninawataka mkaiangalie kwenye eneo la diplomasia ya uchumi na uzoefu wenu vitu gani viongezwe na vipi mnajipanga kwenda nayo diplomasia ya uchumi," aliagiza.

**UTEUZI MTWARA**

Alielekeza Katibu Mkuu mpya wa Mkoa wa Mtwara, Bahati Geuzye, kusimamie utendaji katika mkoa huo hasa miradi ya maendeleo ili kuchochea maendeleo ya eneo hilo.

Alisema alitengua uteuzi wa katibu tawala aliyekuwapo Mtwara baada ya kuona hana nguvu ya kutosha kwenda na kasi ya serikali ya kugeuza mkoa huo kuwa kitovu cha biashara kusini mwa Tanzania.

Pia alimtaka Katibu Tawala mpya wa Mkoa wa Geita, Mohamed Gombati, kushirikiana na mkuu wa mkoa huo kuchochea maendeleo.

Rais Samia pia aliwaelekeza wakuu wa taasisi kumpelekea taarifa za watendaji katika maeneo yao ya kazi ili pale anapofanya mabadiliko, asiwaondoe watendaji wazuri na kuwapeleka sehemu nyingine.

"Huyo kijana niliyemwondoa TTCL (Peter Ulanga) kumbe alishafanya kazi nzuri sana, baadaye mwenyekiti wake wa bodi anasema 'angalia alichokifanya'," Rais alisema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliwaelekeza wateule hao kwenda kuunganisha nguvu za kiutendaji katika maeneo yao ya kazi ili kukamilisha utekelekezaji wa shughuli za kiserikali na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Pia aliwataka mabalozi kwenda kuitekeleza dhamira ya Rais ya kuimarisha diplomasia ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ili kuendeleza uhusiano uliopo kati ya Tanzania na nchi nyingine.

"Mheshimiwa Rais ameweka nguvu sana katika diplomasia ya uchumi. Tunahitaji kutumia fursa za uhusiano tulionayo na maeneo mnayokwenda katika kuimarisha uchumi wetu pia," alisema.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alimshukuru Rais Samia kwa kuwekeza katika nguvu kazi na kumwahidi kuangaza diplomasia na kuongeza hadhi, sifa na heshima ya nchi ulimwenguni.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema watafanya kazi usiku na mchana kutumikia Watanzania kwa kusikiliza kero zao na kuzitatua.

## Mwanafunzi amjeruhi mwalimu kwa panga kwa kumtaka akanyoe ndevu

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Tamabu, Stanford Magaya, amejeruhiwa kichwani kwa kukatwa na panga na mwanafunzi, Alex Butawantemi.

Mwanafunzi huyo amemjeruhi mwalimu huyo kwa kumkata na panga kisogoni akiwa ofisini, baada ya kumrejesha nyumbani kwa ajili ya kwenda kunyoa ndevu na kuvaa viatu.

Baada ya kurejea kutoka nyumbani, mwanafunzi huyo wa kidato cha tatu katika shule hiyo iliyoko Sengerema mkoani Mwanza, aliamuriwa kurudi nyumbani kwenda kunyoa na kuvaa viatu, kama ilivyo utaratibu, baada ya kuwa amevaa kandambili.

Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Samwel Edward, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi kwamba baada ya mwanafunzi huyo kurejeshwa nyumbani ili arudi na sare kamili ya shule, alirejea akiwa ameficha panga katika shati la shule.

"Alifika na kuingia ofisini kwa mwalimu huyo na kumkuta akiendelea kuandaa notisi ndipo mwanafunzi huyo alipomwita na kuitika akamweleza kuwa nimekuja tumalizane ile adhabu ambayo umenipatia,"alisema.

Aliendelea kusimulia kuwa mwalimu huyo baada ya kuinua kichwa, aliona kijana amenyanyua panga ili amkate na katika hali ya kujinusuru, mwalimu alijikuta ameachia mikono ya mwanafunzi na mwanafunzi akamkata kichwani upande wa kisogoni.

Edward alisema baada ya kutekeleza tukio hilo, alitaka kukimbia ndipo walimu walipofika na kumkamata kisha kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi wilayani Sengerema ambao walifika na kumkamata.

Wakati mwanafunzi huyo akiwekwa mikononi mwa polisi, alisema mwalimu huyo alipelekwa katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Sengerema ambako anaendelea kupatiwa matibabu huku hali yake ikiendelea vizuri.

Mmoja wa walimu shuleni hapo, Omary Hussein, alilaani tukio hilo na kuimba vyombo vya sheria na serikali kumchukulia hatua stahiki mwanafunzi huyo ili iwe fundisho kwa wengine kwa kuwa alikuwa amedhamiria kufanya hivyo.

Diwani wa Tabaruka, Sospeter Busumabu, alisema tukio hilo ni la kusikitisha na vijana wamekuwa hawana nidhamu kwa kuwa mwalimu ni mzazi wa mwanafunzi na anatakiwa kumheshimu kama ambavyo anawaheshimu wazazi.

Akizungumzia tukio hilo, Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Genoviva Chuchuba, aliwaomba walimu kutokukatishwa tamaa katika utekelezaji wa majukumu yao na kuwataka kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

Chuchuba pia aliwataka wazazi na walezi kuwa makini na watoto wao na kuwafundisha maadili mema pindi wanapokuwa nao nyumbani na si kuwaachia walimu pekee jukumu hilo.

# Jela miezi sita kwa kumjeruhi mwanawe kwa fyekeo

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Singida, imemhukumu Yahya Sungi, Mkazi wa Kitongoji cha Munyu, Kijiji cha Irisya, wilayani Ikungi kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka sita jela baada ya kupatikana na hatia ya kumkata mtoto wake, Selemani Sungi, kwa fyekeo shingoni, begani na mguuni.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Nuru Chiwalo, alidai kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Novemba, 13, 2022 katika Kitongoji cha Munyu, kwa kumfanyia kitendo hicho na hivyo kumsababishia maumivu makali.

Aidha, Chiwalo alidai kwamba baada ya kutenda tukio hilo, mshtakiwa alikamatwa na kupelekwa kwenye ofisi ya kijiji na baadaye kituo kidogo cha polisi cha Sepuka ambako alikaa kwa siku nane kabla ya kufikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa.

Chiwalo alidai kwamba mshtakiwa baada ya kusomewa mashtaka, alikana kutenda kosa hilo ndipo upande wa Jamhuri ulipowasilisha mashahidi saba. Mashahidi wote walithibitisha bila kuacha shaka yoyote kuwa mshtakiwa ndiye aliyetenda kosa hilo ndipo mahakama ilipomkuta kuwa na kesi ya kujibu.

Kwa mujibu wa mwendesha mashtaka, mshtakiwa hakuwa na mashahidi na alijitetea binafsi kuwa hakumpiga mlalamikaji bali majirani zake ambao ana mgogoro nao kwa upande wa ardhi.

Alidai kuwa kutokana na ugomvi baina yao, walichangia kuchochea mgogoro huo hadi kufikishwa kwake katika mahakama hiyo.

Hata hivyo, mwendesha mashtaka alidai kwamba mshtakiwa alimhoji daktari aliyempokea mlalamikaji ili mahakama ifahamu sababu zipi zilizochangia tarehe za fomu ya matibabu ya polisi (PF 3) kuwa tofauti na maelezo yaliyotolewa, hivyo kuiomba mahakama imwachie huru ili akawalee watoto wake.

Kutokana na kutokuwapo kwa kumbukumbu zozote za mshtakiwa kutenda makosa ya nyuma zinazoonyesha mashtaka dhidi yake, Chiwalo aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa kuangalia silaha iliyotumika.

Hata hivyo, wakili wa mshtakiwa aliiomba mahakama impunguzie adhabu kutokana na kutokuwa na wazazi na pia alikuwa amekaa rumande kwa miezi 11.

Akitoa hukumu, Hakimu Mkuu Robert Oguda alisema kwa kuzingatia yote yaliyoelezwa kwenye shauri hilo, anamhukumu kwenda jela kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka sita jela.

# TAMISEMI yamaliza utata sakata la mwanafunzi 'feki'

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imemaliza ubishi kuhusu sakata la mwanafunzi 'feki' wa kidato cha tano, aliyejiita Sifika Daniel Ruben, ambaye ameiteka mitandao ya kijamii kwa siku mbili mfululizo, akidai ameporwa haki ya kujiunga na tahasusi ya PCM katika Shule ya Sekondari ya Kitaifa ya Namwai, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro.

Mwanafunzi huyo aliyekimbilia kutafuta kazi za ndani jijini Dar es Salaam, amezua gumzo, baada ya shule husika kudai anawahadaa watanzania ili atumie jina hilo ambalo si lake.

Taarifa iliyotolewa Septemba 25, 2023 na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Nteghenjwa Hosseah, ilisema wizara hiyo imebaini kuwa binti anayelalamika mtandaoni anaitwa Sifael Tawel Elirehema na sio Sifika Daniel Ruben.

Sehemu ya taarifa hiyo inaelezwa kuwa, Sifael alisoma Shule moja na Sifika Daniel Urassa, na namba yake ya mtihani ilikuwa ni S 850/135 na alipata Daraja la IV. 34 (zero) na alisoma masomo ya sanaa.

Sifika Daniel Ruben, mwenye namba yake ya mtihani ni S 850/136 alisoma masomo ya Sayansi na alipata Daraja la I. 10.



"Binti anayelalamika mitandaoni alifikishwa shuleni hapo na wazazi/walezi akiwa hana vitambulisho vyovyote (result slip), na alipohojiwa alibainika aliwadanganya wazazi/walezi wake kuanzia jina mpaka matokeo yake na kwa sababu walezi wake hao walimchukua kama msaidizi wa kazi wa nyumbani hawakufahamu ukweli wa taarifa walizopewa na binti huyo."

Aidha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amewataka wazazi/walezi na wanaharakati kutokusambaza taarifa ambazo hawajajiridhisha na usajili wake ili kuepuka kuzua taharuki kwenye jamii.

Miaka mitatu iliyopita tukio kama lililotokea mkoani Mara ambako mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Kiagata, wilayani Butiama Mkoa wa Mara, Mwita Juma Machango, alimjeruhi kwa panga mkononi mwalimu wake Majogoro John, baada ya kupewa adhabu kutokana na utoro.

Mwalimu huyo awali alimwita mwanafunzi wake ili ampatie barua ya kumwita mzazi wake kutokana na tabia yake ya utoro jambo ambalo alikaidi.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mke wake

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imemhukumu Ally Balanda kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia mkewe, Sela Kondo.

Mahakama hiyo iliyoketi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Franko Kiswaga, aliyepewa mamlaka ya nyongeza, ilifikia hatua hiyo baada ya kujiridhisha kwamba upande wa mashtaka umethibitisha kosa bila kuacha shaka.

Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Grace Mwanga na upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Roman Lamwai.

Mshtakiwa anadaiwa Mei 6, 2019 maeneo ya Tabata Liwiti, kwa makusudi alimuua Sela Kondo. Mshtakiwa alikana mashtaka na kwamba yeye na marehemu waliishi pamoja kwa miaka saba kama mke na mume. Katika ushahidi, ilidaiwa walikuwa hawana maelewano kwa muda mrefu ndipo Kondo alipoamua kuhama na kwenda kupanga.

Siku ya tukio, inadaiwa Kondo alitoka na mwanawe, Ashura Shabani (8), kwenda kukutana na mshtakiwa na walipokutana naye, mshtakiwa alimwambia mtoto akanunue juisi dukani anamazungumzo na mama yake.

Mtoto huyo ambaye ni shahidi wa pili, alikwenda dukani lakini alimsikia baba yake wa kambo akiwa anamwomba msamaha mama yake.

Alidai kuwa alipokuwa anarudi alisikia kuna msuguano mama yake alikuwa anaondoka kwenda nyumbani, baba yake alifuata nyuma ya mama yake na alimwona baba akitoa kisu na kumchoma mama yake katika bega la kushoto kisha kukimbia.

Mtoto aliomba msaada watu walisogea, polisi walifika eneo la tukio na kukuta mwili wa Kondo ukiwa unavuja damu maeneo ya shingoni.

Hakimu Kiswaga alisema uchunguzi ulibainisha kwamba Kondo alichomwa na kitu chenye ncha kali.

"Kuna mambo hayabishaniwi, mshtakiwa alikiri aliishi na marehemu kwa miaka saba. Kutokana na msuguano marehemu aliondoka nyumbani akaenda kupanga, walipokutana kulitokea kutoelewana mshtakiwa akamfuata kwa nyuma marehemu.

"Mshtakiwa alikana kuhusika na mauaji hayo na katika utetezi alijitetea mwenyewe hakuwa na shahidi," alisema Hakimu na kuongeza kuwa upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi wanane na kielelezo kimoja.

Katika utetezi wake, mshtakiwa alidai hakuwa akijua kama Kondo alifariki dunia hadi Mei 8, 2019 alipofikishwa polisi. Alidai alipofikishwa mbele ya mlinzi wa amani hakuzungumza kitu na alikuwa na uvimbe katika jicho.

Akisoma hukumu, alisema hakuna ubishi kwamba Kondo alifariki dunia, kifo chake kilisababishwa na kuchomwa na kitu chenye ncha kali na mashahidi walieleza walivyofika eneo la tukio na walimwona anavuja damu kwenye bega.

"Swali la kujiuliza ni iwapo mshtakiwa alimchoma kisu marehemu na kusababisha kifo chake, "Ushahidi wa mtoto ambaye ni shahidi wa pili unaungwa mkono na mashahidi wengine wote, ushahidi wa shahidi wa pili ni ushahidi wa moja kwa moja.

"Kitendo cha mshtakiwa kuwa na kisu kabla ya mauaji inaonekana alikuwa na dhamira ya kumuua marehemu. Mahakama imejiridhisha kwamba upande wa mashtaka umeweza kuthibitisha kosa bila kuacha shaka, shtaka limethibika, Mahakama inamtia hatiani mshtakiwa kwa kosa aliloshtakiwa nalo," alisema Hakimu Kiswaga.

Wakili Mwanga akitoa taarifa za mshtakiwa kabla ya kupewa adhabu alidai hana kumbukumbu ya makosa mengine lakini anaiomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Wakili Lamwai aliomba mteja wake apunguziwe adhabu kwa kuwa ni mkosaji kwa mara ya kwanza na familia inamtegemea.

Akitoa adhabu hiyo, Hakimu Kiswaga alisema mahakama imezingatia kwamba mshtakiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza, anategemewa, amekaa gerezani zaidi ya miaka minne lakini hakuna nafuu iliyotolewa kwenye kosa la mauaji zaidi ya adhabu ya kunyongwa hadi kufa.

"Mahakama kwa kutumia kifungu namba 322(2) cha Sheria ya Makosa ya Jinai, inamhukumu mshtakiwa kunyongwa hadi kufa," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
26.09.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **30.09.2023 hadi 06.10.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya Dar Es Salaam kuelekea Mzenga, gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB15200 DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | Mita | 36.50 |
| Upana | - | Mita | 7.40 |
| Kimo | - | Mita | 4.70 |

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam hadi Mzenga** kupitia **Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro mpaka Mlandizi,** magari yatasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri).*** Kutoka ***Mlandizi kwenda Mzenga*** magari yatasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217619402

# UNFPA, Uingereza zasaidia bil. 23.8/- uzazi wa mpango

**Na Halfani Chusi**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) kwa kushirikiana na serikali ya Uingereza, limetoa vifaa tiba na dawa za uzazi wa mpango vyenye thamani ya Dola za Marekani 9,519,235 (sawa na Sh. 23,845,683,675), kwa lengo la kuokoa vifo vitokanavyo na uzazi.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa jana na Mwakilishi Mkuu wa UNFPA nchini, Mark Schreiner, kwa Mkurugenzi wa Afya ya Uzazi na Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Dk. Ahmed Makuwani, katika hafla iliyofanyika makao makuu ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali ya Tanzania, Uingereza na UNFPA.

Schreiner alisema wameamua kusherehekea Siku ya Uzazi wa Mpango Duniani iliyofanyika jana kwa kutoa msaada huo kama ishara ya kuunga mkono juhudi za Wizara ya Afya kuhamasisha uzazi wa mpango na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Alisema uzazi wa mpango ni muhimu kwa taifa lolote lile kwa sababu unampa nafasi mwanamke kuchagua ni lini azae mtoto na apate watoto wangapi kwa nafasi.

Uzazi wa mpango, alisema pia unahusisha usawa wa kijinsia, pamoja na kumwezesha mzazi kupata nafasi ya kumsomesha vizuri mtoto wake na kupunguza gharama za maisha.

Mkurugenzi wa Maendeleo Ubalozi wa Uingereza nchini, Kemi Williams, alisema uzazi wa mpango ni haki za binadamu na hivyo kila Mtanzania anapaswa kuzingatia ili kupata kizazi salama.

Ofisa Mwandamizi katika Programu za UNFPA ya Afya ya Uzazi Mtoto na Kijana, Felister Mayala, alisema dawa hizo zikitumika vizuri kwa mwaka, zinaweza kuzuia vifo 1,900 vitokanavyo na mimba zisizotarajiwa, kuepusha vifo vitokanavyo na utoaji mimba usio salama kwa watu zaidi ya 400,000.

Akizungumza baada ya kupokea vifaa hivyo, Dk. Makuwani alishukuru kwa msaada huo huku akisisitiza kuwa utasaidia juhudi za serikali kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi hadi kufika sifuri.

Alisema uzazi wa mpango unamsaidia mama kunyonyesha mtoto kwa ukamilifu, kupata taifa lenye watoto wenye akili waliozaliwa kwa nafasi na afya njema.

"Takwimu zilizopo zinaonyesha tumepiga hatua sana kwenye eneo hilo, uzazi wa mpango ni muhimu kuhakikisha mama anakuwa na afya bora," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge (kushoto), akifurahia jambo na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Emmanuel Humba (wapili kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma (watatu kushoto), Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, SACP Ramadhani Ng'anzi (kulia) na Kamanda wa Kikosi hicho Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ACP William Mkonda, baada ya ufunguzi wa kikao kazi baina ya mfuko na wakuu na wakaguzi wa polisi usalama barabarani wa wilaya za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, mjini Kibaha, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tovuti ya nyaraka za Dk. Salim kuzinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

TOVUTI ya hifadhi ya nyaraka za Dk. Salim Ahmed Salim, mwanadiplomasia mashuhuri aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tano na Katibu Mkuu wa Nane wa Jumuiya ya Muungano wa Nchi za Afrika (OAU) kuanzia mwaka 1989 – 2001, inatarajiwa kuzinduliwa Jumamosi jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na familia ya Dk. Salim, mgeni rasmi wa tukio hilo anatarajia kuwa Rais wa Samia Suluhu Hassan.

Viongozi wengine wanaotarajiwa kushiriki ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Wengine ni viongozi waandamizi kutoka sekta za umma na binafsi, viongozi wastaafu na wawakilishi wa washirika wa maendeleo, asasi za kiraia na taasisi za elimu ya juu.

"Tovuti hii (www.salimahmedsalim.com) inajumuisha video, picha na nyaraka mbalimbali (kama vile hotuba, nakala za mawasiliano ya kimaandishi na machapisho ya kitafiti) za Dk. Salim.

"Inatoa ujuzi wa kipekee kuhusu safari yake ya utumishi wa umma, na mchango wake katika mahusiano ya kimataifa na jitihada za ukombozi barani Afrika. Inaangazia mchango wa nchi za Afrika katika siasa za kimataifa katika kipindi cha mwaka 1960 hadi 2000," ilibainishwa katia taarifa hiyo ya familia.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa tovuti hiyo imeandaliwa na familia ya Dk. Salim kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na ndugu, jamaa na marafiki.

Pia, ilibainisha kuwa tovuti hiyo ambayo ni hifadhi ya matukio yaliyotengeneza maisha ya Dk. Salim na muhimu zaidi hifadhi ya nukuu na nyaraka zake mwenyewe, inalenga kuimarisha historia ya Tanzania na ile ya Afrika.

"Nyaraka za tovuti hii zitawavutia wale wanaotaka kuelewa mchango wa Tanzania na wa nchi nyingine barani Afrika katika historia ya dunia na siasa za kimataifa," ilibainishwa katika taarifa hiyo ya familia.

# Wachimbaji: BoT kununua dhahabu kutaongeza wigo

**Na Pilly Kigome,** GEITA

BAADHI ya wachimbaji wa madini wamesema uamuzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kununua dhahabu utaongeza wigo wa soko la madini hayo nchini.

Awali benki hiyo ilikuwa ikihifadhi na kutunza akiba ya nchi kupitia fedha za kigeni (dola), lakini hivi karibuni ilitangaza kuanza kununua dhahabu na kuhifadhi kwenye mfuko wa dhamana za hifadhi za nchi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini yanayoendelea katika viwanja vya EPZA mkoani Geita, walisema sasa wana uhakika wa kupata soko.

Mmoja wa wachimbaji hao ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wanawake Tanzania (TAWOMA), Semeni Malale, alisema hatua hiyo itawezesha kuwa na soko la uhakika la dhahabu.

"Kuna wachimbaji wengi wanawake ambao wanajishughulisha na uchimbaji dhahabu katika maeneo mbalimbali ya Tanzania, hiki walichofanya BoT kitaleta manufaa makubwa kwetu. Tutakuwa na uhakika wa soko la dhahabu, lakini pia kupata bei nzuri," alisema Malale.

Mchimbaji mwingine kutoka Nyankumbu mkoani Geita, Mussa Kisoke, aliyeanza shughuli za uchimbaji mwaka 2010, alisema ana matumaini hatua hiyo ya BoT itaongeza ufanisi katika shughuli zao.

Kwa mujibu wa Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, walianza kununua dhahabu Septemba 21, mwaka huu hatua itakayoiwezesha nchi kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

"Ununuzi wa dhahabu utawezesha kukua kwa shughuli za kiuchumi, lakini pia itakuwa njia mbadala kuweka akiba ya nchi badala ya kutunza fedha taslimu," alisema Tutuba.

Kadhalika, alisema BoT ilishanunua kilo 418 za dhahabu kutoka kwa wachimbaji wa ndani na kuipeleka Uingereza kwa ajii ya kuisajili kwenye soko la dunia na kuhifadhi dhamana kimataifa.

Alisema wana dhamana ya kusimamia masuala ya ukuaji wa uchumi na uhimilivu wa bei pamoja na mzunguko wa fedha na kwa mara ya kwanza toka nchi ipate uhuru walikuwa wakitunza akiba ya nchi kwa mfumo wa fedha za nje.

Gavana huyo alisema dhahabu hiyo itanunuliwa kutoka kwa wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa nchi nzima ikiwamo na wauzaji wengine.

Alisema kabla ya kuhifadhiwa itapelekwa kusafishwa kwenye viwanda vilivyopo nchini kikiwamo GGR cha mjini Geita chenye uwezo wa kusafisha dhahabu kwa asilimia 99.999 ambayo ni sawa na kutoa dhahabu kwa asilimia 100.

"Hatuwezi kupata hasara kabisa kwani kabla ya kuhifadhi tunaisafisha na tunapata dhahabu kwa kiwango hicho, hivyo ondoeni dhana ya kuwa benki itapata hasara kama ilivyokuwa kwa benki zingine," alisema.

Alisema BoT inatumia maonyesho hayo kutoa elimu kwa wachimbaji na wadau wengine ili waweze kupata utambuzi wa namna watakavyouza dhahabu hizo kwenye benki hiyo.

Alifafanua BoT itanunua dhahabu kulingana na bei ya soko kwa siku husika tofauti na wanunuzi wengine ambao inawezekana haziwanufaishi wauzaji.

Aliwashauri wachimbaji na wafanyabiashara kutumia mifumo ya kielektroniki kupokea na kutoa fedha badala ya kutuma fedha taslimu kuepuka ubadhirifu wa kitapeli.

Vilevile, wameanzisha mfumo wa TIPS ambao unaunganisha benki zote na kampuni za simu kwa lengo la kuepuka fedha bandia na kupata malipo papo kwa papo na kwa gharama nafuu.

Aliwashauri wachimbaji kuwekeza kwenye benki hiyo kwa hati fungani na dhamana za serikali kisha watapewa mkataba ambao una thamani sawa na kiwango walichoweka na kuendelea kupata faida.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alipongeza BoT kwa uamuzi huo na kuitaka kuendelea kuwaunga mkono wachimbaji ili kuleta tija na kuongeza mchango katika sekta ya madini.

TANGAZO

# HATIFUNGANI YA KIJANI CRDB: Njia sahihi ya uwekezaji kukuza ujumuishi wa kifedha na uendelevu

**Na Mwandishi Wetu**

KWA uwekezaji wa kuanzia Sh. 500,000, Mtanzania yeyote au asiye Mtanzania anaweza kuwekeza katika Hatifungani ya Kijani ya Benki ya CRDB.

Kupitia hati fungani hiyo, Benki ya CRDB inalenga kukusanya Sh. bilioni 780 katika miaka mitano ijayo, ambazo zitawekezwa katika miradi ya uhimilivu na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa makadirio ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), bara la Afrika linahitaji kati ya dola za Marekani bilioni 20 na 30 kila mwaka ili kufadhili upunguzaji wa athari za mabadiliko ya tabianchi.

Na hili lilibainishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo wakati wa ufunguzi wa awamu ya kwanza ya hatifungani hiyo ya miaka mitano mapema mwezi huu.

Katika awamu ya kwanza, Benki ya CRDB ambayo imeorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na ni benki kubwa kwa upande wa rasilimali, inatarajia kukusanya Sh. bilioni 55 ambazo zitatumika kufadhili miradi ya kijani mipya na inayoendelea.

Hadi sasa, jumla ya nchi 19 duniani zimetoa hatifungani za kijani, huku nchi mbili tu za Afrika; Misri na Tanzania zikifanya hivyo.

"Serikali itachukua hatua muhimu ikiwa ni pamoja na kutunga sera, sheria na kanuni ili kuhakikisha nchi inanufaika na fursa hii ya Hatifungani ya Kijani," alisema Waziri Mkumbo, akisisitiza hatifungani hiyo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

Waziri huyo alisema malengo ya Dira ijayo ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ni kukuza uchumi, ajira na kutengeneza mali, kuongea mauzo ya nje na kukuza maendeleo endelevu.

Alisema utoaji wa Hatifungani ya Kijani ya Muda wa Kati (MTN) ambayo ni sehemu ya Programu ya Dola za Marekani milioni 300, unaashiria hatua kubwa ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2020/21 - 2029/30, ambao ni mwongozo wa kimkakati kuwezesha ujumuishi wa kifedha na ukuaji wa sekta za umma na binafsi.

Akizungumzia mauzo ya hatifungani hiyo, Mkuu wa Masoko ya Kimataifa wa Benki ya CRDB, Burton Mwasamengo, alisema hatifungani hiyo ya bilioni 780 itatolewa kwa awamu. Kiwango cha bei ya mauzo na matumizi ya fedha kitatolewa kulingana na miongozo inayozingatiwa katika utoaji hatifungani.

Anasema awamu ya kwanza itakuwa ya Sh. bilioni 40 na nyongeza (green shoe option) ya Sh. bilioni 15.

Anasema awamu ya kwanza itakuwa ya Sh. bilioni 40 na nyongeza (green shoe option) ya Sh. bilioni 15. Ilianza kutolewa Agosti mwaka huu na itafungwa Oktoba 6 mwaka huu kabla ya kuorodheshwa katika DSE Oktoba 27 mwaka huu.

Hatifungani hiyo itauzwa katika matawi yote ya Benki ya CRDB yaliyosambaa nchi nzima na fomu za maombi zinapatikana katika tovuti ya benki hiyo.

Kiwango cha riba cha asilimia 10.25, ambacho kitalipwa kila mwaka, kimesamehewa Kodi ya Zuio, kitalipwa mwezi Aprili mwakani. Tarehe ya mwisho ya hatifungani hii kuiva itakuwa Oktoba 2028.

Anataja maeneo ya uwekezaji ni kilimo, majengo, miradi ya majisafi na majitaka, nishati jadidifu na usafirishaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, anasema kwa kuanzia Sh. 500,000, mtu au taasisi anaweza kununua hatifungani hiyo.

Anasema uamuzi wa kutoa hatifungani hiyo umetokana na mahitaji makubwa ya mikopo pamoja na mwelekeo wa dunia katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Athari za mabadiliko ya tabianchi zimezigusa jamii nyingi duniani hivyo kulazimu kuunganisha nguvu za kukabiliana nazo. Mafuriko, ukame na mlipuko wa magonjwa ni baadhi ya matokeo ya mabadiliko haya ya hali ya hewa ambayo hatifungani ya kijani inakusudia kuwezesha miradi ya kukabiliana nayo. Nchi nyingi duniani zinatoa hatifungani hizi na sasa ni zamu yetu hivyo namwomba kila Mtanzania kujitokeza kuwekeza ili kwa pamoja tuyalinde mazingira yetu.

"Benki ya CRDB imeweka rekodi ya kuwa taasisi kubwa ya fedha nchini kupata kibali cha kuuza Hatifungani ya Kijani, lakini hili si jipya kwa benki yetu katika uwezeshaji miradi ya utunzaji wa mazingira kwa sababu Novemba 2019, ilitambuliwa na kuingia mkataba na Mfuko wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (GCF) ili kufanikisha miradi ya kulinda mazingira," Nsekela anasema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama, anaipongeza Benki ya CRDB kwa kufanikiwa kuitoa na kuiuza hatifungani hiyo inayokidhi vigezo vya kimataifa vya hatifungani za kijani.

"Ni matumaini yangu kwamba miradi mingi ya kimazingira itanufaika na fedha zitakazotokana na mauzo ya hatifungani hii. Nitumie fursa hii kuzihamasisha taasisi nyingine za fedha, mashirika ya umma na kampuni binafsi kutoa hatifungani zitakazosaidia kufanikisha maendeleo ya taifa letu," anasema Mkama




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Uwekezaji na Mipango Prof Kitila Mkumbo wakijadili jambo na Afisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Abdulmajid Nsekela wakati wa uzinduzi wa Kijani Bond katika uzinduzi uliofanyika jijini Dar es Salaam katika Hoteli ya Serena*




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Uwekezaji na Mipango Prof Kitila Mkumbo (katikati), Afisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Abdulmajid Nsekela (kulia) na Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Mitaji na Dhamana Nicodemus Mkama (kushoto) wakiwasili katika sherehe ya uzinduzi wa Kijani Bond jijini Dar es Salaam katika hoteli ya Serena*




*Mkurugenzi wa Mawasiliano ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation Tully Esther Mwambapa akizungumza katika uzinduzi wa Kijani Bond*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Uwekezaji na Mipango Prof Kitila Mkumbo (watano kushoto), Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Mitaji na Dhamana Nicodemus Mkama, Afisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Abdulmajid Nsekela (watano kulia) wakiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya CRDB Benki Dk Ali Laay (watatu kushoto), Mwenyekiti wa CRDB Bank Foundation Martin Warioba (kulia) na Mjumbe wa Bodi ya CRDB Benki Dk Fred Msemwa (wapili kushoto), Boniface Mhegi (watatu kulia), Miranda Naiman (wapili kulia) na Katibu wa CRDB Benki John Rugabo (kulia)*

CRDB BANK
The bank that listens

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Mtaka kuhusu unyonyeshaji ni mwafaka

**WIKI** iliyopita, Kanisa la Waadventista Wasabato liliadhimisha Sikukuu ya Vibanda ambayo ilihitimishwa mwishoni mwa wiki.

Sikukuu hiyo ilifanyika mkoani Njombe na Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, ndiye alifungua na kufunga.

Mkuu huyo wa Mkoa, wakati akifunga sikukuu hiyo, alizungumza mambo kadhaa lakini kubwa alikemea tabia ya baadhi ya kinamama kukwepa jukumu la kuwanyonyesha watoto wao kwa kisingizio cha kufanya kazi za kujiongezea kipato. Kutokana na kuwapo kwa tabia hiyo, alilitaka kanisa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kunyonyesha kwa ajili ya afya bora ya mtoto.

Mtaka alitoa mfano wa Mkoa wa Njombe kwamba wanawake ndio wanaoongoza katika kumiliki uchumi, lakini wamekuwa na shida katika kuwanyonyesha watoto wao kwa muda unaotakiwa. Baadhi ya wanawake katika mkoa huo, alisema baada ya kujifungua hupika makande na kuyaacha ndani wiki nzima na watoto, wakiwamo wanaotakiwa kunyonya maziwa ya mama, kula chakula hicho kuanzia asubuhi mpaka jioni, aidha Mtaka alikemea vitendo hivyo kwa kuwa matokeo ya hayo yote ni watoto kukumbana na matatizo kiafya yakiwamo ya udumavu na utapiamlo.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, aliwaomba viongozi wa kanisa hilo, kuwaelimisha wanawake kuhusu umuhimu na faida za maziwa ya mama kwa mtoto ikiwamo kuwaandaa wakati wa ujauzito na miaka mitano ya kwanza. Kauli hiyo ya Mtaka inasadifu hali halisi ya sasa kuhusu udumavu na utapiamlo kwamba pamoja na mikoa kama Iringa na Njombe kuwa vinara katika uzalishaji wa chakula, bado inaongoza kwa tatizo hilo.

Kila mwaka Tanzania imekuwa ikiungana na nchi zingine duniani kuadhimisha Wiki ya Kimataifa ya Unyonyeshaji ambayo pamoja na mambo mengine hutumika kuwahimiza na kuwakumbusha kinamama umuhimu wa kuwanyonyesha watoto katika miezi 0 hadi sita bila kuwalisha chakula chochote. Hali hiyo inatokana na takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba takriban asilimia 40 ya watoto wachanga wenye umri huo pekee ni wanaonyonyeshwa kikamilifu.

Pamoja na hayo ijulikane kwamba maziwa ya mama yana manufaa makubwa kwa afya na ukuaji wa mtoto na kwamba kama watoto walio chini ya miaka mitano watanyonyeshwa kikamilifu wanaweza kunusurika dhidi ya maradhi mbalimbali kwa kuwa miili yao inakuwa imejengeka vyema kutokana na maziwa na vitamini nyingi ambazo ni kinga dhidi ya maradhi hasa yanayowakumba watoto.

Unyonyeshaji maziwa ya mama kwa mtoto unatiliwa mkazo kwa sababu pamoja na mambo mengine, yanachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa mtoto na kuongeza uzito wa mwili unaotakiwa lakini kubwa zaidi humsaidia mtoto kuboresha uwezo wa utambuzi wa akili (IQ), mahudhurio ya shule na pia huhusishwa na mapato ya juu katika maisha yake ya utu uzima.

Hata hivyo, faida ya unyonyeshaji si kwa mtoto pekee bali hata kwa mama kwa kuwa kufanya hivyo kwa muda mrefu pia huchangia afya na maisha bora ya mama kwa kuwa humpunguzia hatari ya kupata saratani ya mfuko wa mayai ya uzazi na matiti.

Ni vyema kama alivyosema Mtaka, wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini wasaidie kutoa elimu kuhusu unyonyeshaji kwa ajili ya afya na makuzi bora ya watoto kwa ustawi wao wa baadaye. Kwa kufanya hivyo kutaepusha matatizo mbalimbali kwa watoto kama ilivyobainishwa na Shirika la Save the Children kuwa matatizo mengi ya watoto ukiwamo utapiamlo, husababishwa na kutonyonyeshwa ipasavyo na inakadiriwa kuwa vifo vya watoto milioni 2.7 kwa mwaka duniani hutokana na tatizo hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Wabongo acheni kuchezea umeme

**KILIO** cha mgawo wa umeme kinachotikisa kila kona ya nchi, pamoja na serikali na TANESCO kupasua kichwa jinsi ya kupata nishati ya uhakika, walaji tunapaswa kubadilika kimatumizi.

Ninachosema, baadhi ya wateja wanaotumia umeme kana kwamba ni kitu kisichokuwa na mwenyewe au gharama mfano joto au mwanga wa jua.

Wengine huwasha umeme saa 24, tena wanatumia taa au balbu zinazokula umeme mwingi bila kujali kuwa nishati hiyo si jua inagharama ikihitaji uwekezaji na fedha nyingi mno.

Ni ukweli usiopingika kuwa makundi yenye matumizi kuanzia kampuni, wazalishaji bidhaa viwandani na mashambani mfano wazalisha vifaranga na wafugaji.

Wengine ni wafanyabiashara wa maji kwenye visima ambao hutumia pampu kuyapandisha maji katika ardhi na kuyaingiza matangini.

Pia lipo kundi lingine la wafanyabiashara wa maduka maeneo ya mijini, ambao wamekuwa wakiwasha taa muda wote kwa mwaka mzima bila kuzima kutokana na maelezo kuwa wanaishi mbali na biashara zao, wanaamini ulinzi ni taa kuwaka mchana na usiku.

Wafanyabiashara wengine wanachojali ni kuweka pesa ili LUKU iwe na umeme wakiwasha taa majira yote.

Sio hao tu bado kuna kundi jingine ambalo hutumia vifaa vilivyochakaa kama majokofu na hata mifumo ya waya iliyochakaa inayopoteza umeme.

Vifaa hivyo hutumika kwa muda wote wa saa 24 hata mwaka bila kujali kuwa ulaji wake wa umeme unakuwa mkubwa na unaathiri gridi ya taifa.

Pamoja na kwamba ni wateja wa TANESCO wanaonunua umeme kulingana na matumizi yao lakini mbali na hilo, wakumbuke wanatumia fedha nyingi kwa matumizi hayo pia umeme huo mwingi wanaotumia unazalishwa kwa kutumia maji kwenye mabwawa, gesi na mafuta kwenye vinu hivyo kukausha gridi ya taifa na matokeo yake ni mgawo.

Athari za mgawo huo ni kubwa, kwanza zinaongeza gharama za uzalishaji viwandani na ndani ya kampuni.

Ikumbukwe kuwa kubwa zaidi ni kukosekana maji licha ya ukweli kuwa jamii haioni haraka maji ya uhakika majumbani yatakuwa kazi kutokana na mitambo ya kuyasukuma kutoka kwenye vyanzo kutegemea umeme

Wawekezaji wakumbuke kuwa kama kampuni haikuwa na bajeti ya tahadhari ya umeme na kuweka akiba ya kununua mafuta kuendesha jenereta, ni tatizo.

Wafanyakazi watakosa mishahahara na mambo mengine yatakwama.

Kwenye saluni vinyozi watalazimika kufunga kutokana na mashine kutegemea umeme, kwenye maduka ya kitoweo ya nyama, samaki na kuku zinazohifadhiwa kwenye majokofu changamoto ni kubwa nao bila jenereta wanalazimika kufunga milango.

Ikumbukwe shida inakwenda hadi kwenye biashara ya maziwa, maduka makubwa ya dawa zikiwamo chanjo za mifugo na binadamu wanakumbwa na hasara hiyo ambayo inadhoofisha uwekezaji wao na kutishia kufilisika.

Kwa matatizo ya sasa ni wakati wa wafugaji hasa wa kuku na mifugo mingine wanaotumia umeme saa 24 kuanza kubadilika kwa kusaka nishati mbadala hasa umeme jua.

Wafunge kwenye mabanda yao na kuuwasha kwa saa kadhaa kwa kadri wanavyotaka.

Ujumbe huu uwafikie wafugaji wanaofunga taa zinazokula umeme mkubwa na mwanga mwingi na zenye joto kwa kisingizio kuwa vifaranga na kuku waweze kuona vizuri, kula na kukua haraka.

Anasahau kuwa unapotokea mgawo kama sasa anaathirika na wenzake wanaowasha taa chache ambazo zinatunza umeme au energy server.

Ikumbukwe kuwa taifa linapoingia kwenye mgawo wa umeme, TANESCO inapata hasara kubwa kwa kukosa mapato kutokana na ukweli kuwa hakuna biashara.

Hivyo, ni bora wenye matumizi makubwa ya umeme, wajirekebishe waangalie uwezekano wa kutumia sola.

Kubana matumizi na kulinda umeme pia kuwa ajenda, ofisi za umma, binafsi na familia au nyumbani watu wazime umeme si kuwasha taa mwaka mzima.

# Masauni akerwa wahalifu watoto kusumbua wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, amelitaka Jeshi la Polisi nchini kubadilika na kujiandaa kupokea mageuzi makubwa yaliyofanywa na serikali ikiwa ni mapendekezo ya wataalamu kutoka katika vyombo vya ulinzi na usalama ili kudumisha amani na kuzuia uhalifu wa aina mbalimbali nchini.

Alitoa rai hiyo jana baada ya kusikiliza kero kutoka kwa wananchi wa eneo la Bububu wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika Shehia ya Kijichi, Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja, baada ya kufanya kikao cha ndani na uongozi wa Jeshi la Polisi visiwani humo.

“Rais Samia ameanza kuleta mabadiliko makubwa katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, ametoa ajira na kupandisha vyeo askari akitaka jeshi lishuke chini kwa wananchi ili kupambana na uhalifu kuanzia ngazi ya kata.

Hapa wananchi wamezungumza mambo mengi wakilituhumu Jeshi la Polisi, nawataka kubadilika kupambana na uhalifu, haiwezekani wahalifu tena watoto wadogo wasumbue wananchi, wakati jeshi hili limekua na historia ya kupambana na matukio makubwa ya uhalifu, nawaagiza badilikeni.”

Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi linapowapeleka mahakamani watuhumiwa wa makosa mbalimbali ya uhalifu huku akisisitiza ulinzi shirikishi kuboreshwa katika jamii.

“Kumekuwapo na changamoto ya baadhi ya wananchi kushindwa kufika mahakamani kutoa ushahidi polisi wanapopeleka watuhumiwa mahakamani hali inayosababisha mahakama kutoendelea na kesi, hapa tuna kesi takribani watu saba...” alisema Kamishna Hamad.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Magharibi A, Mary Isungi alisema jumla ya majalada 13 yameondolewa mahakamani baada ya mashahidi kushindwa kutokea mahakamani huku akikiri hali hiyo inasababisha wahalifu wengi kurudi mtaani na kuendelea na matukio ya uhalifu ikiwamo kuwaingilia watoto kinyume na maumbile, unyang’anyi wa kutumia silaha, kunajisi, kubaka na kuvunja maduka kwa dhamira ya kutenda kosa la wizi.

---


**Faidika**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE COMPANIES ACT, CAP 212 R.E 2002

LETSHEGO TANZANIA LIMITED T/A FAIDIKA

REGISTRATION NO. 52622

NOTICE OF MEMBER'S VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY

**NOTICE** is hereby given to the General Public that on the 18th day of September 2023, the members of Letshego Tanzania Limited, T/a Faidika passed Special Resolution for voluntary winding up the company in terms of the provision of Section 334 (1) of the Companies Act [Cap 212 R.E. 2002].

This **NOTICE** is hereby issued to all parties concerned and to the General Public.

STELLA JOSIAH MANONGI.
CHAIRPERSON

DIANA NGOMUO
SECRETARY

217619102

Tanzania | Vodacom Towers – Paloma Park 3rd Floor, Plot 23 Ursino Estate | P.O. Box 6137 | Dar es Salaam | Tel: (+255) 22 222 5029 | Fax: (+255) 22 212 4856
A subsidiary of Letshego Holdings Limited (Reg No. Co 98/422). Letshego Tanzania Limited Registration No. 52622 of 2002
Letshego Holdings Limited is listed on the Botswana Stock Exchange ISIN BW 000 000 1247
Executive Directors: P. Segadimo (CEO), Non-Executive Directors: S. Manongi (Chairperson), C. Mloka (Tanzania), D. Mugashe (Tanzania), G. Almeida (Tanzania)

www.letshego.com/tanzania (+255) 22 222 5029 (+255) 754 451 388 Letshego Tanzania T/A Faidika faidika_tanzania tz.faidika@letshego.com


---


Government electronic payment gateway https://billing.gepg.go.tz/payments/show/21681748658[illegible]

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

United Republic of Tanzania

**Prime Minister's Office - Government Printer**

Exchequer Receipt

**Stakabadhi ya Malipo ya Serikali**

| | |
|---|---|
| Receipt No | : **923268204177456** |
| Received from | : LETSHEGO TANZANIA LIMITED T/A FAIDIKA |
| Amount | : 20,000.00 |
| Amount in Words | : Twenty Thousand TZS And Zero Cent(s) Only |
| Outstanding Balance | : 0.00 |

| In respect of | Item Description(s) | Item Amount |
|---|---|---|
| *142101030006 - Printing and Publications - REG. 52622* | 20,000.00 | |
| | **Total Billed Amount :** | **20,000.00 (TZS)** |

| | |
|---|---|
| Bill Reference | : 47312268233429539846 |
| Payment Control Number | : ***994730032077*** |
| Payment Date | : **2023-09-25 13:16:44** |
| Issued by | : Alphonce Gwaje |
| Date Issued | : 2023-09-25 13:19:18 |
| Signature | : |

Government Payment Gateway © 2017 All Rights Reserved (GePG)

For: GOVERNMENT PRINTER ACCOUNTS

217619102

9/17/2023, 11:35 PM


---


**Faidika**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
THE COMPANIES ACT CAP 212 R.E 2002
LETSHEGO TANZANIA LIMITED

SPECIAL RESOLUTION OF MEMBERS OF THE COMPANY PURSUANT TO SECTION 333(1) (b) OF THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2002

**At a duly convened and constituted Extra Ordinary General Meeting of the Members of the Company that was held on 18th September, 2023, Members of the Company unanimously RESOLVED as follows:**

That Letshego Tanzania Limited Trading as Faidika be placed in the voluntary winding up under the provision of section 333(1) (b) of the companies Act, Cap 212 R.E 2002.

CERTIFIED TRUE EXTRACT

CHAIR PERSON

SECRETARY

19th Sept 2023
DATE

217619102

Tanzania | Vodacom Towers – Paloma Park 3rd Floor, Plot 23 Ursino Estate | P.O. Box 6137 | Dar es Salaam | Tel: (+255) 22 222 5029 | Fax: (+255) 22 212 4856
A subsidiary of Letshego Holdings Limited (Reg No. Co 98/422). Letshego Tanzania Limited Registration No. 52622 of 2002
Letshego Holdings Limited is listed on the Botswana Stock Exchange ISIN BW 000 000 1247
Executive Directors: P. Segadimo (CEO), Non-Executive Directors: S. Manongi (Chairperson), C. Mloka (Tanzania), D. Mugashe (Tanzania), G. Almeida (Tanzania)

www.letshego.com/tanzania (+255) 22 222 5029 (+255) 754 451 388 Letshego Tanzania T/A Faidika faidika_tanzania tz.faidika@letshego.com

# Kizimbani mashtaka kujifanya ofisa serikalini, kulaghai polisi

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

ALEXANDER Matesi mkazi wa Sengerema, mkoani Mwanza, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Sengerema kwa mshataka ya kujifanya ofisa wa serikali wilayani hapa na kujaribu kulaghai baadhi ya maofisa wa Jeshi la Polisi.

Baada ya kupandishwa kizimbani, Matesi alisomewa mashtaka matatu ya kumdanganya ofisa wa polisi kuwa yeye ni ofisa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, kumdanganya Mkuu wa Usalama Barabarani kuwa ni ofisa wa ngazi za juu na kumtaka wajadili masuala ya kiserikali na kujifanya Katibu Tawala wa Wilaya.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Sengerema, Tumsifu Barnabas, Mwendesha Mashtaka wa Jeshi la Polisi, Mkaguzi wa Polisi Nyamhanga Mayadi, alidai mtuhumiwa alitenda makosa tajwa kwa nyakati tofauti.

Alidai kuwa katika kosa la kwanza, mnamo Julai 6 mwaka huu, mshtakiwa alikwenda kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Sengerema na kuomba ahadi ya kukutana naye kwa ajili ya kufanya naye kikao na kueleza kuwa yeye ni mfanyakazi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Alidai kuwa kati ya Juni hadi Julai mwaka huu, visivyo halali, Matesi alijifanya ofisa wa juu serikalini na kwenda kwa Mkuu wa Usalama Barabarani wilayani Sengerema, Khamis Wembo, na kumwomba kujadili masuala ya serikali.

Vilevile, katika kipindi cha mwezi Juni hadi Julai mshtakiwa huyo alijifanya Katibu Tawala wa Wilaya ya Sengerema na kujaribu kufanya utapeli kinyume cha sheria.

Mshtakiwa huyo baada ya kusomewa mashtaka hayo, alikana kutenda makosa hayo. Mahakama iliamuru arudishwe mahabusu mpaka Oktoba 5, mwaka huu kesi hiyo itakapoitwa kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali.



Mfamasia na Mchambuzi wa Sera kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Regina Richard, akichangia hoja katika mjadala wa maadhimisho ya Siku ya Wafamasia Duniani, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## RITA: Mwarobaini migogoro kifamilia ni kuandika wosia

**Na Happy Severine,** BARIADI

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umesisitiza Watanzania kujenga tabia ya kuandika wosia kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kwa kiwango kikubwa kuepusha migogoro ya mara kwa mara katika familia na kuwezesha warithi halali kupata haki yao kwa wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign) inayoendelea mkoani Simiyu, Ofisa Sheria kutoka RITA, Grace Shao, alitaka jamii kuacha woga kuandika wosia.

Alisema kuwa kufanya hivyo si uchuro na kusema baadhi ya watu wameandika na wanaendelea kuishi vizuri huku waliondika na kupoteza maisha, familia zao zimeendelea kuishi bila migogoro.

"Familia nyingi zimekuwa na migogoro ya mara kwa mara juu ya mirathi, wengine wamedhulumiwa na ndugu ambao kisheria siyo warithi wa mali. Tumeendelea kuwaelimisha wananchi kuwa mwarobaini wa haya ni wosia," alisema.

Ofisa sheria huyo alitaka wananchi kutumia taasisi ya RITA kuandaa wosia kwa kuwa ni chombo cha serikali, pia ni taasisi ambayo haina ukomo wa maisha na ina wanasheria wabobevu wa masuala ya wosia na mirathi.

Alihimiza wazazi kujenga tabia ya kuwatafutia vyeti vya kuzaliwa watoto ili kuondoa usumbufu wanaooweza kupata pindi watakapotakiwa kwenda kuanza shule na kuhitaji cheti cha kuzaliwa.

Alisema kuwa kwa sasa mtoto akitakiwa kwenda kuandikishwa shuleni, ni lazima awe na cheti za kuzaliwa. Kupata cheti cha kuzaliwa ni muhimu katika kufanikisha kupatia bima ya afya.

"Tunawasihi wananchi mtoto akizaliwa, ndani ya siku 90 ni muhimu kumtafutia cheti cha kuzaliwa, hii itasaidia kumtengenezea mtoto msingi mzuri wa majina yake pamoja na kumbukumbu yake ya tarehe za kuzaliwa," alisema.

RITA inaendelea kutoa huduma ya usajili na kutoa vyeti vya vya kuzaliwa, elimu ya mirathi, kuandika na kuhifadhi wosia kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayoendelea katika Viwanja vya Stendi ya zamani mjini Bariadi.

## Kamishna wa Madini aonya ununuzi wa madini bila leseni

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

KAMISHINA wa Madini, Dk. Abdulrahman Mwanga ameonya watu wanaonunua madini bila leseni kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Alitoa onyo hilo jana kwa niaba ya Waziri wa Madini, Anthony Mavunde wakati wa mafunzo kwa wachimbaji wadogo katika ukumbi wa EPZ eneo la Bomba mbili mkoani Geita.

Alisema mtu yeyote akibainika anamiliki madini bila kuwa na leseni, atanyang'anywa madini na hata kufilisiwa na kufungwa gerezani kwa kuwa utaratibu unaelekeza ili upate haki ya kuchimba madini, hatua ya awali unatakiwa kuwa na leseni.

Alisema lengo lao ni kutoa elimu kwa wananchi ili wajue si halali kufanya shughuli za madini bila kuwa na leseni.

"Tunalichukua hili suala ili tuwafuatilie hawa watu ambao wanafanya hizi shughuli bila kufuata utaratibu wa kuwa na leseni ili tuwachukulie hatua zinazositahili," alisema.

Kamishna wa Madini alisema atahimiza ofisi za ofisa madini mkazi kote nchini kuwapa wananchi elimu juu kuhusu upatikanaji leseni kwa urahisi.

"Ni hatari kufanya shughuli hizi bila kuwa na leseni. Hatujachoka kutoa hii elimu na nina uhakika wanaofanya shughuli kama hizi siyo wengi, wako wachache. Lakini, bado tunahitaji kuwaelimisha ili wasifanye shughuli hizi, kwa sababu wao ni chanzo cha utoroshaji madini," alisema.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema Maonesho ya Teknolojia ya Madini yatakapohitimishwa Septemba 30 mwaka huu, atabaki Geita ili kushughulikia malalamiko kuhusu shughuli za uchimbaji madini zinazosababisha nyumba kupasuka.

# Uhaba wa vyoo watishia usalama wa wanafunzi

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

ZAIDI ya wanafunzi 460 wa Shule ya Msingi Kivava iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, wanalazimika kutumia matundu sita ya choo kutokana na shule hiyo kukabiliwa na uhaba wa miundombinu hiyo.

Kutokana na dosari hiyo, baadhi ya wanafunzi hulazimika kurejea nyumbani kujisaidia huku baadhi yao wakijisitiri vichakani. Imeelezwa na uongozi wa shule hiyo kuwa matundu sita yaliyoko shuleni, pia yana hali mbaya ya uchakavu, hivyo yanahatarisha usalama wa wanafunzi.

Jana Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Innocent Shomari, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari shuleni huko kuhusu changamoto mbalimbali zinazoikabili kwa muda mrefu sasa.

Alisema, mahitaji ya matundu ya vyoo katika shule hiyo kwa sasa ni kati ya matundu 16 na 20, lakini wanayo sita pekee ambayo hayakidhi mahitaji ya wanafunzi.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, tundu moja la choo linapaswa kutumiwa kwa uwiano wa wanafunzi 20 wa kike au 25 wa kiume, hivyo wanafunzi 460 wa shule hiyo wanahitaji matundu 18 ya choo kukidhi mahitaji ya kisera.

Mwalimu Shomari alibainisha kuwa matundu sita yaliyoko shuleni yana hali mbaya ya uchakavu, yana nyufa na sakafu yake ina dalili za kubomoka na kuhatarisha usalama wa wanafunzi.

"Tuna uhaba mkubwa wa matundu ya vyoo shuleni. Kwa sasa tuna matundu sita tu ambayo yanatumiwa na zaidi ya wanafunzi 460 wakati mahitaji ni matundu zaidi ya 16 mpaka 20, lakini pia hata haya yaliyopo sita yapo katika hali mbaya sana na yana nyufa za kutaka kubomoka, hivyo tunaiomba serikali itujengee matundu ya vyoo," alisema.

Mwalimu Shomari alisema Kijiji cha Kivava, iliko shule hiyo, kilikumbwa na mafuriko mwezi April mwaka huu na hivyo miundombinu ya choo kuharibiwa .

Mwalimu huyo pia alisema shule inakabiliwa na dosari ya uhaba wa vyumba viwili vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la awali na la pili. Wanafunzi wa madarasa hayo kwa sasa wanasomea nje.

"Pia tuna changamoto ya madawati, tunayo madawati 78 pekee kwa sasa, hivyo tunahitaji msaada wa madawati," alisema.

Kisera, dawati moja katika shule ya msingi linapaswa kutumiwa na wanafunzi watatu, hivyo shule hiyo yenye wanafunzi 460 inapaswa kuwa na madawati 153.

Mwenyikiti wa Kamati ya Shule hiyo, Saidi Makua alieleza kuwa baada ya kuona hali mbaya ya vyoo, changamoto hizo zinashughulikiwa na uongozi wa kijiji kwa kiwango chao wakati wakisubiri fungu kutoka serikalini.

Ofisa Elimu Wilaya ya Mtwara, Devis Kasembe alisema ana taarifa za hali hiyo shuleni na tayari halmashauri imeshatenga bajeti kwa ajili ya utatuzi.



# Suma JKT kujenga nyumba 5,000 waliokubali kuhama Ngorongoro

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wamesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Suma JKT, kujenga nyumba 5,000 za wakazi waliojiandikisha kuhama kwa hiari ndani ya eneo la NCAA.

Akizungumzia jana wakati wa makubaliano hayo, Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk.Freddy Manongi, alisema ujenzi wa nyumba hizo awamu ya pili utaanza Oktoba Mosi mwaka huu na utakamilika ndani ya miezi sita.

"Nichukue fursa hii kuwashukuru sana JWTZ kusani Suma-JKT kwa ushirikiano wao katika kutekeleza mradi huu," alisema Dk. Manongi.

Alisema zoezi la kuhamisha wananchi lilipoanza Juni 2022, hadi sasa tayari makundi 19 yenye kaya zaidi ya 565 sawa na watu 3,097 na mifugo zaidi ya 15,500 imeshahama ndani ya hifadhi.

Kadhalika, Dk.Manongi alisema hamasa ya wananchi kujiandikisha kuhama kwa hiari imeendelea kuongezeka na hadi sasa jumla ya kaya 1,524 zimejiandikisha kuhama.

Vilevile, alisema serikali itaendelea kuhamasisha wakazi wa Ngorongoro walioomba kuhama kwa hiari kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu.

Aidha, alisema kwa awamu ya pili nyumba hizo zitajengwa katika maeneo ya Saumu na Kitwayi na alieleza kuwa kipindi hiki watajenga nyumba yenye vyumba vitatu vya kulala.

Naye Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, alitumia fursa hiyo kushukuru kwa kukabidhiwa jukumu la kujenga nyumba hizo kwa awamu ya pili.

Alisema awamu ya kwanza katika ujenzi wa nyumba 503 JKT walipewa kazi ya kujenga nyumba 402 katika kipindi cha miezi tatu hadi kukamilika kwake.



Imamu wa Masjidi Raudhia Kazamoyo, katika Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Issa Hotti (kushoto), akizungumza kuhusu umuhimu wa elimu wakati wa mahafali ya darasa la saba ya wanafunzi wa kiislam wa shule za Tafara ya Moipo, hivi karibuni. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanahabari kusaidia kompyuta Shule ya Msingi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI ya Wanahabari ya Kusaidia Jamii za Pembezoni (MAIPAC) imeahidi kutoa msaada wa kompyuta kwa Shule ya Msingi ya Arusha Alliance, ambayo ili kuwezesha wanafunzi kusoma masomo ya TEHAMA.

Mkurugenzi Mtendaji wa MAIPAC, Mussa Juma alitoa ahadi hiyo jana wakati wa mahafali ya darasa la saba ya 14 ya shule hiyo, ambapo ni moja kati ya shule 10 bora katika Jiji na Arusha zinazoongoza kila mwaka kwa kufaulisha.

Juma ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mahafali hiyo, alisema shule hiyo ni mfano wa kuigwa nchini kwa sababu imeanzishwa na walimu baada ya kuamua kuungana na kuchangishana fedha.

Alisema kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani, elimu ya TEHAMA ni muhimu kwa wanafunzi kuanzia shule za msingi.

Juma ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi katika Vyombo vya Habari Tanzania (JOWUTA), aliwataka wahitimu kuendelea kuwa na maadili ambayo ndio yatasaidia kufanya vizuri katika maisha yao.

Kadhalika, aliwataka walimu nchini kuiga mfano wa walimu wa Alliance kuungana na kuanzisha shule yao, kwani kuna wadau wengi wa kuwaunga mkono ikiwamo serikali na taasisi za fedha.

Kaimu Mkuu wa shule hiyo, Elimboto Mdiu alisema shule hiyo, iliazishwa mwaka 2007 ikiwa na wanafunzi 18 tu lakini sasa ina wanafunzi 800.

Mdiu alisema katika mahafali hayo wanafunzi 114 wamemaliza darasa la saba, ambapo wasichana ni 56 na wavulana 48.

Awali Diwani wa Kata ya Olasiti, Alex Martin alisema kata yake inajivunia shule hiyo kwani imekuwa ikiongoza kufanya vizuri, lakini pia kutoa elimu na maadili mazuri kwa wanafunzi.

# Wakazi Muheza wakosa maji siku 40 wamlilia DC

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKAZI wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, wamelalamika kukosa maji kwa muda wa wiki tano na kumuomba Mkuu wa Wilaya kuingilia kati kuimaliza kero hiyo.

Maeneo ambayo yamekumbwa na shida hiyo ni Kijiji cha Kilapula, Ngomeni Moja, Bagamoyo, Mkanyageni, Tanganyika na Lusanga.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe wakazi wa Kijiji cha Mkanyageni wilayani Muheza wamesema wamekuwa wakitumia maji ya bwawa kutoka Kijiji cha Umba, jambo ambalo linahatarisha usalama wa afya zao.

Mkazi wa kijiji hicho, Maleko Shayo alisema takribani wiki tano sasa hawana maji, wanawake wanalala visimani kutafuta maji bila mafanikio na wahusika wa TANGA-UWASA hawaelezi shida ipo wapi.

"Hapa kilio chetu kikubwa ni kero ya maji na kwa sasa tunatumia maji ya Bwawa la Kijiji cha Umba. Hii ni hatari na ndiyo maana mara nyingi tunaugua magonjwa ya tumbo, alisema Maleko mkazi wa Kijiji cha Mkanyageni.

Mkazi wa Kijiji cha Mkanyageni, Selemani Jumanne alisema kuwa kero hii ya maji imedumu miaka mingi, hawajui tatizo liko wapi.

Alisema kuwa hivi sasa wananunua maji dumu kwa Sh. 1,500 kutoka kwa walanguzi wanayatoa Tanga mjini, kwamba kwa sasa kilio chao wanakipeleka kwa Mkuu wa Wilaya na mbunge.

Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki alisema kutokana na malalamiko ya wananchi hao tayari amewasiliana na wahusika kutoka TANGA- UWASA.

Alisema ameshawaagiza kuhakikisha wanafanya kila njia kuhakikisha huduma ya maji inarejea kwa wananchi.

# Mjane adai kutaka kupokwa mali, amlilia Rais Samia

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MJANE Devota Stephano (68), mkazi wa Moivaro, Jijini Arusha, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, aingilie kati sakata la mtoto wake wa kufikia, Amani Mollel, anayetaka kumdhulumu maeneo aliyoachiwa na marehemu mumewe.

Kwa mujibu wa mjane huyo (Amani) baada ya kumaliza kuuza maeneo yake ya urithi aliyopewa na marehemu, amegeukia mali zake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana nyumbani kwake Mtaa wa Sekei, mjane huyo alimtuhumu (Amani), kutumia nafasi yake ya kazi vibaya kumnyanyasa kwa kuwa yeye hana kipato.

Alisema kuwa Amani alifungua kesi ya madai katika Mahakama ya Mwanzo Maromboso Arusha na baadaye Mahakama ya Wilaya na aliwahi kukata rufaa Mahakama Kuu lakini mahakama zote hizo alishindwa kwa kukosa udhibitisho wa madai yake.

"Baada ya kuona nimemshinda mahakamani aliende ofisi za RITA ambao walikuja na kuanza kupima mali za marehemu. Pia amekuwa akiandika barua za kuzuia wazee wa ukoo wasitumie eneo la mila akidai ni mali yake, akitaka kuliuza kinyume cha sheria". alisema

Alisema aliolewa kwa ndoa halali na marehemu mwaka 1980 wakati huo marehemu alikuwa akiishi Kondoa na alikuwa akifanya kazi ya udereva Wizara ya Elimu.

Mjane huyo alisema wakati anaolewa alimkuta mumewe ana watoto watatu wa mke wa kwanza ambaye aliachana naye mwaka 1979, miongoni mwa watoto hao ni pamoja na Amani, Rehema na Godfrey huku rehema akiwa mtoto wa kwanza.


Mjane alisema kabla ya kifo cha mumewe mwaka 2017, marehemu alifanikiwa kugawa mali zake yakiwemo mashamba kwa watoto wote pamoja na yeye.

Alisema Amani alipatiwa maeneo lakini baadaye aliyauza na mwaka mmoja baada ya kifo cha marehemu alianza kuyataka maeneo mengine ambayo siyo mali yake.

Nipashe lilimtafuta Amani kwa njia ya simu ambaye alisema hawezi kuzungumzia suala hilo kwa kuwa lipo mahakamani jambo linalopingwa na mjane akisema hakuna kesi yoyote iliyopo mahakamani, huku akionesha nakala za hukumu za kesi hizo zilizoamuliwa mwaka 2021.

"Hilo suala lipo mahakamani mimi siwezi kujibu chochote ni suala la kisheria nisije nikapotoka nikaeleza suala ambalo halipo" alisema Amani.

Hata hivyo alipotakiwa kueleza ni kesi gani ipo mahakamani na mahakama ipi alikata simu na hakuweza kupokea tena.



# ‘Ukikamatwa hutoi risiti faini mil.1.5/- itakuhusu’

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Tabora imetangaza vita dhidi ya wafanyabiashara wanaokwepa taratibu za ulipaji kodi kwa kutokutoa risiti wakati wa mauzo na manunuzi.

Imesema kuwa yoyote atakayekamatwa atatozwa faini ya Sh. milioni 1.5 au asilimia 20 ya bidhaa iliyouza.

Meneja wa TRA Mkoa wa Tabora, Fredrick Kanyilili wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa licha ya kutozwa kwa faini hiyo vilevile mhusika atachukuliwa hatua nyingine za kisheria.

Alisema kuwa wafanyabiashara wanawajibu wa kutoa risiti halali wanapofanya mauzo ya bidhaa katika maeneo yao ikiwa ni sehemu ya ulipaji kodi kwa kila bidhaa inayouzwa kwa serikali.

Kadhalika, aliwataja wanunuzi wa bidhaa katika maeneo mbalimbali kuwa ni lazima waombe risiti halali iliyoorodhesha idadi ya bidhaa pamoja na gharama sahihi ya bidhaa hiyo aliyoinunua.

“Mnunuzi ambaye hatodai risiti vilevile atatozwa asilimia 20 au kulipa faini ya Sh.30,000 kwa kosa la kukiuka taratibu za kisheria,” alieleza.

Aidha, alisema TRA katika Mkoa wa Tabora itaendesha kampeni ya tuwajibike kuhakikisha wanafuatilia utoaji wa risiti duka hadi duka na kwenye biashara zao.

Hata hivyo, alisema pia watakuwa wanachukua hatua kwa wale wote watakaobainika kwa watakaotoa risiti ambazo siyo halali au wateja ambao wamenunua bidhaa bila kupata risiti.

Alisema kwamba kampeni hiyo imezinduliwa mwanzoni mwa wiki hii katika mkoa huo ikiwalenga wafanyabiashara wote hasa kwenye biashara korofi ambazo zimekuwa changamoto katika utoaji wa risiti kwenye maduka ya jumla, vifaa vya ujenzi baa, hoteli na nyumba za kulala wageni.

Naye Meneja Msaidizi TRA, Musa Sudi alikiri kuwa mashine za kutoa risiti wakati mwingine inaweza kusumbua kimtandao au kuharibika, hivyo wanatakiwa wafanyabiashara kutoa taarifa.

Alisema mtumiaji wa mashine hiyo anatakiwa kuiwasilisha kwa aliyemuuzia na kutoa taarifa ofisi ya TRA iliyopo karibu na yeye ndipo atarudhusiwa kutumia kitabu cha mkono.

Sudi alisema pindi mashine itakapotengenezwa risiti alizozitoa kwa mkono atapaswa kuziingiza kwenye mashine hiyo.




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (kushoto), akiwa katika stoo ya dawa ya zahanati ya Seseko, Mwamalili Manispaa ya Shinyanga, kabla ya kuweka jiwe la msingi na kuifungua rasmi juzi. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# RC Mndeme aonya wizi wa dawa hospitalini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amewaonya watumishi wa afya kutokujihusisha na vitendo vya wizi wa dawa katika maeneo yao ya kazi.

Alitoa angalizo hilo juzi wakati akifungua na kuweka jiwe la msingi katika Zahanati ya Seseko iliyopo Mwamalili Manispaa ya Shinyanga, kuanza kutoa huduma za matibabu kwa wananchi.

Alisema katika ukaguzi wake alioufanya katika stoo ya dawa ya zahanati hiyo amebaini uwepo wa dawa za kutosha, hivyo kuwaonya baadhi ya watumishi wanaotarajia kufanya wizi wa namna yoyote wa dawa hizo.

“Nimejionea mwenyewe wingi wa dawa zilizopo katika zahanati hii isije ikapotea hata panado, hakikisheni zinawafikia walengwa wanaokuja kupatiwa matibabu na yeyote atakaye jihusisha na wizi wa dawa na kubainika atachukuliwa hatua kali za kisheria,” alieleza Mdeme.

Kadhalika aliwaonya watumishi wa afya kuacha tabia za matumizi ya simu ‘kuchati’ wakati wakiwahudumia wagonjwa lengo likiwa ni kuwapatia huduma stahiki wagonjwa na wahitaji wa huduma husika.

Alisema katika mkoa huo Sh. bilioni 33 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya, hivyo maelekezo yake ni kutaka kuona ubora wa huduma hizo zinaendana sambamba na matibabu kwa wananchi.

Katika hatua nyingine aliumagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, kuhakikisha katika Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga kuna jenereta ya dharura ili umeme ukikatika huduma za matibau ziendelee kutolewa na kutosababisha uhalibifu wowote wa dawa na chanjo ambazo huwekwa kwenye majokofu.

Aidha, Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Seseko, Dk. Briliance Ombay, akisoma taarifa ya ujenzi wa zahanati hiyo, alisema umegharimu Sh.milioni 95.6 na inatoa huduma za matibabu kwa wananchi 2,741.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga, Dk. Pierina Mwaluko, akisoma taarifa ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura katika hospitali hiyo, alisema serikali ilitoa Sh.milioni 500 lakini mpaka sasa wametumia Sh.milioni 292 na ujenzi upo hatua za mwisho na ukamilishaji.

# Wachimbaji madini wapewa hadhari kuhusu afya zao

**Na Alphonce Kabilondo,** Geita

WACHIMBAJI pamoja na wananchi wanaojishughulisha na shughuli za uchimbaji wa madini mkoani Geita wameshauriwa kuwa na utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara ili kulinda afya zao kutokana na athari za kemikali na vumbi.

Wito huo umetolewa juzi na Daktari kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Chato, Dk.Liberius Libent , wakati akiongea na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya teknolojia ya madini yanayoendele mkoani humo.

Alisema kuwa kemikali na vumbi hilo ni chanzo cha matatizo ya upumuaji yanayowakabili kwa kiasi kikubwa wachimbaji na wananchi wanaofanya shughuli zao katika maeneo ya migodi.

Kadhalika, aliwataka wachimbaji wadogo kuhakikisha wanatumia vifaa kinga wakati wa shughuli za uchimbaji madini lengo likiwa ni kupunguza au kudhibiti kabisa madhara hayo ya kiafya.

Dk. Liberius alisema kuwa tangu maonyesho yaanze wamewahudumia watu 150 ambapo kati yao 38 wamekutwa na matatizo ya ugonjwa wa moyo na upumuaji, sababu kubwa ikiwa ni kutokana na shughuli za uchimbaji bila ya kuchukua tahadhari.

Alisema kuwa ushiriki wao katika maonyesho ya sita ya teknolojia ya madini umelenga kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo, kwamba Hospitali ya Kanda Chato inaendelea kutoa elimu kwa wananchi hasa kwa wanaojihusisha na uchimbaji wa madini .

Mmmoja wa wananchi waliofika katika banda hilo kupata huduma ya vipimo na ushauri, Tumpe Jonas alieleza kupokea maelekezo ya kuwa na utaratibu wa kupima afya kila mara na kuchukua tahadhari katika shughuli zake, lengo likiwa ni kufanya kazi kwa umakini.

Mkazi mwinginge, Stephano Peter alisema katika maeneo hayo ya uchimbaji elimu juu ya matumizi ya vifaa kwa ajili ya kujikinga haitolewi mara kwa mara akisema baadhi ya wachimbaji wamekuwa wakifanya kazi kwa mazoea hali inayosabisha ongezeko la magonjwa hayo.

Hivyo, aliomba serikali kuweka mkazo katika kuhamasisha upimaji wa afya na kudhibiti hatua za baadhi ya wachimbaji kufanya kazi hiyo kwa mazoea ili kulinda afya zao na nguvu kazi ya taifa.



Ukurasa 12

**UN inaponyong'onyezwa kumbe, malengo endelevu yamepuuzwa**



Ukurasa 13


Kwa mbinu hizi kero wamachinga zitakwisha

siasa

JUMATANO SEPTEMBA 27, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 14

**Ulezi wa Karume na Prof. Babu, kujituma, uanaharakati Afrika miaka 19 alishang'ara**

# Kuabudu itikadi za vyama, kunavyokimbiza kero ikulu

**Na Sabato Kasika**

KATIKA ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, anayoifanya mikoa ya Mtwara na Lindi hivi karibuni, anatuma ujumbe wa kueleza kukerwa na mtindo wa malalamiko ya wananchi kufikishwa Ikulu wakati wasaidizi wake walitakiwa wayashugulikie katika ngazi za chini.

Anawagusa wanaomsaidia hao kuwa ni viongozi kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji hadi mikoa, ambao kiutaratibu wanatakiwa kwanza kushughulikia malalamiko kabla ya kufikishwa ngazi zao kwa ajili ya utatuzi, lakini badala utaratibu huo kuzingatiwa , yanaruka hadi Ikulu.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe inazungumza na wachambuzi na wanasiasa wanaosema chanzo cha hali hiyo ni matokeo ya ushindi wa baadhi ya viongozi uliopatikana 'mezani' katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 na ule mkuu wa 2020.

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdaleba Sakaya, anadai na kuongeza kuwa , katika uchaguzi huo, CCM iliamua kujitwalia ushindi na kuweka watu wasio na uwezo wa kuongoza, na kwamba wamekuwa kero kwa wananchi kwa kushinda kuwatatulia shida zao.

"Mwananchi anakwenda kwa mwenyekiti kitongoji, kijiji, mtaa kata na kwingineko kupeleka malalamiko yake lakini hayatatuliwi, ndiyo maana Rais anashangaa kuona hata kero za kawaida ambazo zingetatuliwa na wawakilishi wake zinafikishwa ofisini kwake," anasema Magdalena.

Anasema ipo haja kwa serikali ya CCM kujifunza jambo ili kuandaa uchaguzi ambao wananchi wanakuwa huru kuchagua viongozi wao wanaowataka na sio kubambikiwa wasiowataka.

"Ninaamini kwamba kama uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 na ule wa wabunge , madiwani na rais 2020 ungekuwa huru wananchi wangechagua viongozi wao ambao wanajua wanaweza kuwasikiliza na kutatua kero zao," anasema.

Naibu Katibu Mkuu huyo anasema njia pekee ya kumaliza kero ya viongozi wasiofanya kazi, ni kuruhusu uchaguzi huru ambao utawafanya wananchi watumie sanduku la kura kuchagua wale ambao wana imani nao.



Rais Samia Suluhu Hassan akiweka jiwe la msingi la Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Lindi iliyoko Kijiji cha Kilangala. **PICHA: IKULU**

Mbunge wa zamani Moshi Vijijini (TLP), Thomas Ngawaiya, anasema itikadi za vyama vya siasa zinachukua nafasi badala ya kuwatumikia wananchi.

"Inawezekana pande zote mbili kati ya wananchi na viongozi wao zina matatizo, lakini kikubwa zaidi ninachokiona ni masuala ya itikadi za vyama ndio yanayowahangaisha viongozi wetu," anasema Ngawaiya.

Anafafanua kuwa baadhi ya viongozi wanafanya kazi kwa kuzingatia itikadi za vyama, na kwamba mwananchi ambaye ni wa chama tofauti na mlengo wake anaweza kupeleka kero kwa kiongozi ambaye si wa chama chake asimsikilize na kusababisha malalamiko.

"Itikadi za vyama ni sehemu ya tatizo, baadhi ya viongozi hawasikilizi kero za watu, kwa sababu si wa chama chao. Watu wa aina hii hawafai kupewa madaraka," anasema Ngawaiya ambaye sasa ni mwana CCM.

Aidha, uwezo mdogo wa utendaji kazi wa baadhi ya viongozi ni tatizo huku akitolea mfano mkurugenzi wa halmashauri moja kwamba Wizara ya Maji iliwahi kuingiza fedha katika akauti ya halmashauri kwa ajili ya uchimbaji wa malambo, lakini akazirudia wizarani.

"Ninadhani ipo haja kwa wanaoteuliwa wawe waelewa wa mambo mbalimbali, ili wafanye kazi yao kwa ufanisi, sio kwenda kujifunza,ni vyema wapimwe uwezo wao kwanza kabla ya kupewa uongozi," anasema.

Ngawaiya anagusia suala la wananchi kubeba mabango yenye malalamiko yao kwa mamlaka kuu kama Rais , Waziri Mkuu au Makamu wa Rais ni ishara kwamba kuna jambo haliko sawa kati yao na viongozi wao.

"Siku hizi kero kubwa imekuwa ni migogoro ya ardhi, ambayo unaweza kukuta viongozi wao ndio chanzo, hivyo si rahisi kutatua kama wao ndiyo wahusika wakuu. Wito wangu ni kwamba wanaoteuliwa wawe ni waelewa ambao watamsaidia Rais kufikisha kule anakotaka," anasema Ngawaiya.

**INAENDELEA UK. 12**

# UN inaponyong'onyezwa kumbe, malengo endelevu yamepuuzwa

**Na Christina Mwakangale**

MKUTANO wa 78 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA78), unaokutanisha viongozi wakuu wanachama wa UN umehitimishwa jijini New York Marekani baada ya wiki moja ya kutathmini mikakati na mafanikio mbalimbali ya umoja huo, jicho likielekezwa kwenye utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu (SDGs), unaofikia ukingoni 2030.

Miongoni mwa agenda zilizotawala mkutano huo ulioanza Septemba 19, makao makuu ya UN ni kuhusu SDGs, ambayo tangu yawekwe mezani na umoja huo ni miaka takribani nane sasa.

Malengo hayo ni 17 ambayo nchi wanachama 193 wa UN wameyaridhia kuyatekeleza kupitia serikali zao, licha ya kufikia nusu ya safari ya kuelekea mwisho wa makubaliano ya utekelezaji wake mwaka 2030, Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres, anatilia shaka kutimia azma ya SDGs.

Katika ufunguzi wa mkutano huo, Guterres, anasema dunia inahitaji watu na serikali na sio michezo au migogoro, akiungwa mkono na Rais wa Baraza Kuu, Balozi Dennis Francis ambaye hotuba yake ya ufunguzi anabainisha kuwa uwezo na njia za kutatua changamoto upo, lakini hatua hazipo.

"Tuamini katika imani ya kusudi moja na mshikamano wa hatua za pamoja. Amani ni uwekezaji katika ustawi wetu wa pamoja," anasema Balozi Francis.

Nchi za Afrika, hasa zinazoendelea zimeachwa na makovu kutokana na changamoto kadhaa kama vile migogoro ya kisiasa na mapigano kati ya serikali na waasi, janga la UVIKO-19, mafuriko, mabadiliko ya tabianchi, vimechangia kusuasua kwa malengo hayo.

"Kama hatutachukua hatua sasa, agenda ya mwaka 2030 ya malengo yote 17 itakuwa kama maneno yanayoandikwa kwenye kibao kinachowekwa kaburini kumbukumbu ya aliyefariki. Kwa dunia ambayo imekuwepo, tungechukua hatua," anasema Guterres kwenye mkutano huo na kuongeza kuwa wana zana na rasilimali zote za kutatua changamoto za pamoja, wanachohitaji ni uamuzi.



Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, akihutubia Baraza la Umoja wa Mataifa. **PICHA: UN NEWS**

Wakichangia mada mwishoni mwa wiki kwenye redio ya DW wasomi kadhaa wamejadili kauli za viongozi wa dunia na dunia itarajiwayo kutoka mkutano huo wa dunia.

Profesa David Munda kutoka Marekani , anasema kauli za Katibu Mkuu wa UN, Guterres zina uzito unaohitaji tafakuri kama dunia yenye uhai na watu wenye fikra, akisema malengo ya SDGs yanahusisha falsafa toauti za siasa zenye ushindani duniani husan kwa mataifa yenye nguvu.

"Kwa mfano China na Marekani, kuna ushindani kwamba nani atapunguza matumizi yanayochangia kukwama kwa maendeleo, ustawi pia wa nchi hizo ni tofauti kubwa na mataifa mengine. Jamii ya kimataifa inatakiwa kuja pamoja, ili kukabili mabadiliko ya tabianchi.

"Malengo ya SDGs ni mapana na yanahusisha kupunguza umaskini, kuongeza kasi ya uchumi, ila uwiano haupo. Nchi zilizoendelea hazipo tayari kutoa teknolojia yao iliyowafikisha walipo leo , wakidhani wale nao wataendelea, Afrika ni mzigo ni mkubwa zaidi, mapinduzi ya serikali, vita, kule Sudan na Sahel kumewadhoofisha ," anasema Prof. Munda.

Anataja ushirikiano wa kikanda na kimataifa ni muhimu, ikizingatiwa maeneo yaliyo na rutuba kama vile misitu ya DRC ingeweza kuongeza chakula, hakuwezi kupandwa mbegu kutokana na vita.

"Mataifa yaliyoendelea yagawe teknolojia ya kijani, ili kuinua ustawi wa nchi zingine. Hatuwezi kuangalia janga la njaa bila kuangalia ustawi wa kijinsia. Afrika Kusini kuna shida dhidi ya wahamiaji, sisi Waafrika tujiangalie, tunawezaje kushirikiana. Tunasema mabadiliko ya dunia, lakini hao wakuu wa nchi wamesafiri na ndege binafsi hadi New York .....," anahoji Prof. Munda.

Takwimu za UN zinabainisha viwango vya juu vya umaskini kwa watu milioni 575 duniani watakuwa wanaishi kwenye hali duni za maisha uliokithiri huku theluthi moja pekee ya dunia, ndio itafanikiwa kupunguza kiwango cha umaskini kwa asilimia 50 ifikapo 2030.

Katika kuchangia hilo, Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, anasema juhudi bado hazijafanikiwa katika kuondokana na umaskini, ikiwamo kuwapo kwa majanga ya asili kama wiki iliyopita nchi takribani nane zote zilikuwa na mafuriko yaliyoua watu na kuathiri rasilimali.

"Lengo la kwanza, la pili na latu halijafanikiwa, kupunguza umaskini, njaa, kutoa elimu bora na ustawi wa jamii wenye afya, haviwezi kupatikana kwa sababu ya majanga yanayoendelea," anasema Dk. Rose.

Anasema lengo namba 13 la kuchukua hatua za mabadiliko ya tabianchi, ni ngumu kufikiwa kwa sababu wazalishaji wa hewa ukaa kutokana na mapinduzi ya viwanda unahusisha nchi zilizoendelea huku zinazoendelea zikiathiriwa zaidi.

Umoja wa Mataifa unapima viwango vya njaa pia, ukisema mwaka 2022 asilimia 9.2 ya jumla ya wakazi wote duniani sawa na watu milioni 735 walikumbwa na njaa kali kutoka watu milioni 613 waliokuwa na hali hiyo mwaka 2019, katika hilo, Hamisa Zaja, Mratibu wa Maendeleo Maji Kenya na Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi, anasema:

"Mara nyingi nchi zinazoendelea tunawategemea wenzetu walioendelea, lakini mnapokaa meza moja utaona zinataka kusaidia, zina uwezo lakini nyingi zinaangalia maslahi yao. Tunahitaji usawa, ili kujikwamua na lengo la kwanza la kuondokana na umaskini.

"Badala ya kuja kusema tutawasidia mwanzo mjikwamue,wanakuja na vikwazo, sheria ngumu, mkikwama wanakuja na mikopo migumu na wakifikiria riba kubwa. Ni wakati wa nchi zilizoendelea ajenda zenye usawa mezani kwa asilimia 100 kwamba kweli tunataka kusaidiana. Sio kuja na ajenda za siri kukidhi malengo yao," anasema Hamisa.

Baadhi ya malengo ya SDGs ni kutokomeza umaskini, kukomesha njaa, kuwa na afya njema na ustawi, kutoa elimu bora; kuwapo usawa wa kijinsia; maji salama na usafi; nishati mbadala na za gharama nafuu; kuwapo kazi zenye staha na ukuaji viwanda.

Kadhalika malengo mengine ni ubunifu na miundombinu; kupunguza tofauti, kuwa miji na jamii endelevu; kuhakikisha matumizi ya uzalishaji wenye uwajibikaji na kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

## Kuabudu itikadi za vyama, kunavyokimbiza kero ikulu

**INATOKA UK. 11**

**HAWAJIAMINI**

Mchambuzi wa siasa Deus Kibamba, anasema sababu kubwa ambayo inachangia wananchi kufikisha kero zao Ikulu, inatokana na baadhi ya viongozi wa maeneo yao kutojiamini na kushindwa kushughulikia kero na hivyo wananchi kuamua kuzipelekea juu.

Anasema wananchi wana uzoefu wa kupeleka kero kwa viongozi wao lakini hazitatuliwi, hivyo wanaona ni bora wamsubiri Rais, Makamu wa Rais au Waziri Mkuu watoe malalamko yao kwao, baada ya kuona viongozi wao hawayashughulikii.

"Ndio maana mmemsikia Rais Samia akihoji 'hata hili nalo hadi lije Ikulu'. Sababu kubwa ya baadhi ya viongozi kutojiamini inatokana na shida ya kikatiba," anasema na kufafanua kwamba madaraka mengi katika nchi za Kiafrika yamejazana sehemu moja ambayo ni ngazi ya juu na kusababisha viongozi wa chini kutojiamiani wakati wa kufanya maamuzi wakiwa na hofu nyingi.

"Wanahofia kufanya maamuzi wakidhani watawakosea wakubwa wao. Hatua hiyo inasababisha wafanye kazi kwa woga na kuishia kushindwa kufanya maamuzi wanapopelekewa malalamiko," anasema.

Kibamba anaeleza kuwa ni heri kuongozi anayefanya maamuzi akakosea kuliko yule asiyefanya, kwa kuwa asiyefanya maamuzi jamii haiwezi kujua uwezo wake wa utendaji, hasa katika kutoa maamuzi.

Mchambuzi huyo anasema mtu akipewa dhamana ya kumwakilisha kiongozi wa juu sehemu fulani, afanye kazi, na kwamba akikosea atarekebishwa, huku akifafanua kuwa mtindo wa kutofanya kazi wakati wananchi wana kero, hakuna maana ya Rais kuwa na wawakilishi wasiotatua matatizo ya wananchi.

# Kwa mbinu hizi kufukuza wamachinga, kutakwisha



Mtaa wa Congo, Dar es Salaam ni maarufu kwa biashara za wamachinga. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

UKUAJI wa kasi wa miji unaongezeka, wakati huo Dar es Salaam ikitarajiwa kufikia hadhi ya jiji kuu (mega city) ndani ya miaka saba ijayo.

Hayo ni kwa mujibu wa Ripoti za Umoja wa Mataifa za Maendeleo ya Miji (2019), zikioonyesha kuwa Cairo nchini Misri, Kinshasa DRC na Lagos Nigeria tayari ni majiji makubwa, huku Luanda Angola, Johannesburg Afrika Kusini na Dar-es-Salaam zikitarajiwa kupata hadhi hiyo mwaka 2030.

Ni habari njema lakini, inayoweza kuitwa pasua kichwa kisera, kijamii, sheria, huduma za jamii na uchumi. Kuwa jiji kubwa kuna maana ujio wa changamoto zaidi , mathalani majiji hayo yatakuwa na idadi kubwa ya watu tena wenye vipato vidogo wanaokimbilia mijini ndilo ongezeko la makazi duni, uhalifu, uhaba wa ajira, upungufu huduma za afya kama maji, barabara, tiba, nishati na elimu.

Kadhalika ipo athari kiuchumi kama ongezeko kubwa la watu kwa mujibu wa sensa ya 2022 ina wakazi milioni saba. Nyingine ni kupanuka biashara nyingi zisizo rasmi kama kuuza bidhaa ndani na pembeni ya barabara, kuziba njia za wapita njia, vituo vya mabasi na sehemu zote zenye uwazi. Ni changamoto ambayo kiasi inavyokua itashindikana kuikabili.

Kikubwa ni ongezeko la watu na shughuli za kiuchumi zisizo rasmi au 'umachinga' na sasa ndiyo wakati wa taifa kuchukua hatua kiubunifu, kutunga sheria za kuratibu, kusimamia na kulinda uchuuzi na biashara ndogo mijini, anashauri Dk. Donath Olomi, katika mahojiano.

Anasema wamachinga au wachuuzi mijini wanaongezeka na sekta hiyo isiyo rasmi inazidi kukua na kuhitaji udhibiti na usimamizi madhubuti ili kisiwe kikwazo kwa sekta rasmi ya uchumi.

Dk. Olomi, Mtendaji Mkuu wa tasisi ya usimamizi na maendeleo ya ujasiriamali (IMED), anasema mataifa jirani kama Kenya yameanza kuchukua hatua, kuna sheria ya kusimamia na kulinda biashara za wafanyabiashara wadogo wakiwaita Jua Kali, lakini hata Rwanda ipo kadhalika na India.

Anasema India sheria hiyo inasimamia na kuendelea wafanyabiashara wadogo zaidi, wadogo na wa kati na kwamba zinaelekeza wafanyabiashara kujiunga pamoja, kuwa na umoja rasmi unaowasimamia, wakitakiwa kuwa na katiba na kufuata taratibu zote za kisheria na kisera na mifumo zilizoandaliwa.

Anafafanua kuwa sheria inawahusu wafanyabiashara wa tasnia zote iwe ni bodaboda, bajaji, vifaa vya kielektroniki, makondakta na madereva wa daladala, wachimbaji wadogo, mama na babalishe, wauza nguo, mboga na matunda, samaki na hata mafundi ujenzi.

Anasema wote kila mmoja kutoka katika tasnia yake anajisajili kuwa chini ya umoja unaoisimamia kama ni bodaboda, kuuza mitumba au vyakula na kila mfanyabiashara lazima ajisajili na kupewa utambulisho, alipe kodi au ushuru kisheria.

Anaongeza kuwa kupitia umoja huo wafanyabiashara wanapewa masharti na maelekezo, mikataba, masuala ya kodi, usafi , eneo au masoko na kila kitu kinachohusu .

> Wamachinga au madalali kwenye masoko wanawapunja wakulima na kusababisha biashara za rumbesa na kufanyika biashara zisizozingatia vipimo wala mizani za kitaalamu.

Anafafanua kuwa uratibu wake unafanyika kwenye halmashauri na manispaa kwenye ngazi za chini na wote wanaojiunga wanatambulika na wilaya, kata na miji yao kufuata taratibu na sheria kama zinavyoelekezwa na halmashauri.

Dk. Ulomi anasema ili kuwa na sekta hiyo ya wafanyabiashara wadogo iliyosimama ni lazima kuwa na sera, kutunga sheria na kuandaa mifumo ya kiubunifu ya kuwawezesha kujipanga na kujisimamia wenyewe, kazi inayoratibiwa na mamlaka za chini mfano manispaa na halmashauri za miji.

Ili kila eneo liweze kujiongoza, kuwa na utaratibu wa kujisimamia na kulinda haki zake kwa mujibu wa sera, sheria na mifumo ya kiubunifu.

Dk. Olomi mkurugenzi wa kwanza wa kituo cha ujasiriamali UDSM cha (UDBS), mbobezi wa masuala ya ubunifu na ujasiriamali na kuendeleza sekta binafsi, anaeleza kuwa ujio wa sheria utawaweka wachuuzi katika mfumo unaoeleweka na kuondoa kero na vurugu mijini kama ilivyo sasa.

Wachuuzi hao wanatakiwa pia kuwa na chombo au kamati mfano kwenye halmashauri kwa ajili ya kuwashughulikia kwa kila hatua akisema Rwanda kama biashara yoyote haipo kwenye mfumo rasmi hairuhusiwi.

"Lazima wawe wanachama wa kikundi cha uchuuzi wa aina inayokubalika na kutambulika kisheria, kusajiliwa ambacho mwanachama wa kikundi cha kiwilaya. Ripoti na kazi zao zote zifahamike , wapya kwa wageni watambulike pia."

Anasema kuna umuhimu wa kusimamia kisheria sekta hiyo kwa vile inakua biashara hazina leseni, hazilipi kodi, hazina usimamizi na zinatandazwa barabara na hata nje ya maduka ya wale wanaolipa ushuru, kodi na wenye leseni.

### ANGALIZO

Dokta Olomi anaonya kuwa kama uchuuzi mijini hauidhibitiwi unavuruga uchumi rasmi, kwa mfano inawezekana wafanyabiashara wanaolipa kodi wakafunga maduka na kuuza bidhaa kwa utaratibu wa kimachinga.

Kadhalika, hata wengine kuanzisha viwanda kwa kificho na kuzalisha bidhaa vichochoroni zisizolipiwa kodi wala kuingia kwenye mkondo wa uchumi rasmi.

Hili linaweza kutokea kwenye bidhaa zisizolindwa na sheria ya ushindani mfano mafuta ya kula mfanyabiashara anaweza kukamua mafuta ya alizeti na chikichi akauza, lakini vitu kama sementi, sigara na bia haviweza kuzalishwa vichochoroni.

Anaonya kuwa uchuuzi ni kero na wapo wanaokusanyika nje ya maduka na kuzuia biashara rasmi zisifanyike kama wamiliki wanavyotaka.

### MITIZAMO MINGINE

Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam wanaunga mkono serikali kuwaondoa wamachinga mitaani na kwenye maeneo mengine kwa maelezo kuwa uchuuzi umeua mipango ya sekta rasmi.

Wanaungana na Dk. Olomi kuwa umachinga au sekta isiyo rasmi isiyodhibitiwa kisheria, itaendelea kuvuruga karibu kila eneo na kusababisha vurumai na ukiukaji sheria.

Wanatoa mfano maeneo ya makaburi wamiliki ni halmashauri za miji lakini wapo wamachinga maalumu huonyesha maeneo ya kuzikia, kuchimba na kuchukua malipo badala ya mamlaka za miji.

Baadhi ya wanafunzi wa uchumi UDSM, wanasema madalali wanaoibuka kila mahali wanapima viwanja na kuvuruga sheria za mipango miji.Wanawaona hao pia kuwa ni wamachinga kwenye ardhi licha ya kwamba hawapangi bidhaa barabarani, uchuuzi huo kwenye viwanja umesababisha kupima viwanja vidogo na kuvuruga mpangilio wa miji na majiji mengi.

Kadhalika, wamachinga au madalali kwenye masoko wanawapunja wakulima na kusababisha biashara za rumbesa na kufanyika biashara zisizozingatia vipimo wala mizani za kitaalamu. Kwenye mabasi wamesababisha kulangua tiketi na hata kukwamisha mifumo rasmi ikiwamo ya kuuza tiketi kielektroniki.

Kwa upande wake Dk. Peter Kafumu , mbunge wa zamani wa Igunga na Kamishna wa Madini, anasema wamachinga wanatoka kwenye nchi zenye uchumi maskini kama mataifa ya Afrika na mara nyingi ni uchumi usiokwepeka.

Anaeleza kuwa ni eneo linalohitaji ufuatiliaji na udhibiti maana hata juhudi za kuwaendeleza ni ngumu kwa vile wanahamahama na si rahisi kuwapata.

Anatoa mfano, kwenye sekta ya madini kuwa bila kuwapo mifumo, sera na sheria ni vigumu kuwakusanya, kuwapa mikopo na kuifuatilia wairejeshe pamoja na kuwaendeleza kutokana na kuhamahama kukimbiza biashara.

## TOVUTI YAKE MBIONI KUZINDULIWA...
## DK. SALIM AHMED SALIM;

# Ulezi wa Karume na Prof. Babu, kujituma , uanaharakati Afrika miaka 19 alishang'ara

• Kaanzia uandishi, darasa siasa ziarani Cuba...
• China akutana na Waziri Mkuu Chuo En Lai

**Na Peter Orwa**

***WAKATI mwishoni mwa wiki hii kunatarajiwa kuzinduliwa tovuti yenye maelezo ya Mtanzania, mwanadiplomasia gwiji duniani, Dk. Salim Ahmed Salim, Jumatano wiki iliyopita, gazeti hili ilikuwa na simulizi yake, ikiwamo kuteuliwa na Rais Julius Nyerere kutumika kuwa balozi, kijana wa umri miaka 22, siku chache baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Je mzizi wake uko wapi? Pata simulizi....***



Dk. Salim Ahmed Salim. **PICHA: AFP**

KUNA usemi 'usione vinaelea, vimeundwa' ndio unabeba maana kubwa katika maisha ya jamii. Pia, wanataaluma nao wanapoona kuna kisicho cha kawaida, hupenda kusimama kupata siri ya jambo muhimu, kupitia kinachoitwa 'etymology' au mzizi wake.

Ni kawaida, baadhi ya watu wanaonekana kuwa zao bora leo katika jamii na taifa kwa jumla, hata kimataifa, chemchem yao imeibuliwa na waliosimamia maisha yao kabla.

Ndio nadharia zinazoingia katika rekodi binfasi za mwanadiplomsia, Dk. Salim Ahmed Salim, ambaye si wote wanaojua ni zao la bidii, utashi, usimamizi makini na mafunzo ya watangulizi waliotukuka katika za ukombozi Zanzibar, ikizingatiwa hata mwenyewe si muongeaji sana, bali wa vitendo zaidi.

Hapo katika orodha ya waliomuunda, anaingia yule aliyerejea nchini katika miaka ya 1990, akiwa na sifa ya kitaaluma profesa; Abdulharman Mohamed Babu na Rais Muasisi, Abeid Aman Karume.

Dk. Salim baada ya kumaliza shule, akawa kijana mwanaharakati wa uhakika kusaka haki ya wazanzibar, yungali katika umri miaka 19 pekee. Hapo alihamasishwa na maono ya wanaharakati wa kupigania uhuru wa Afrika na hamasa hizo zilikuwa maradufu, hasa baada ya masomo yake.


Hakuficha namna anavyokerwa na jamii ya kiafrika kugawanyika, akitaka umoja zaidi kwao Zanzibar; visiwa vya Unguja na Pemba.

Baada ya kuhitimu darasa la 12 (kidato cha nne), Salim akajiunga na kazi ya uandishi wa habari, mwenyewe akiwa na simulizi ya kilichomsukuma katika jukumu hilo, ni hamasa kuchangia harakati za haki Afrika, katika vita dhidi ya kudai uhuru Zanzibar kutoka katika koloni la Kiingereza.

Hapo ufanisi wake ukampandisha ngazi hadi kuwa Mhariri wa gazeti la chama ZNP na baadaye gazeti kama hilo la chama cha Umma, baadaye gazeti la Sauti ya Vyama Tisa, lililomilikiwa na vyama hivyo.

Ni kipindi hicho akawa Katibu wa Umoja wa Waandishi wa Zanzibar. Hata ilipofika mwaka 1961, akiwa kijana wa miaka 19, tayari alikwishaiva, hata akawa mteule, kati ya vijana watatu wa visiwani kwenda nchini Cuba, katika tukio la kufungua ofisi ya chama ZNP.

> Ni uteuzi ulionyooshewa kidole kutoka kwa viongozi wa ZNP, Abdulrahman Mohamed Babu na Ali Sultan Issa, ambako jijini Havana walifungua ofisi na nyingine jijini Cairo, Misri.



Sheikh Abeid Aman Karume. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Profesa Abdulrahman Mohamed Babu

Ni uteuzi ulionyooshewa kidole kutoka kwa viongozi wa ZNP, Abdulrahman Mohamed Babu na Ali Sultan Issa, ambako jijini Havana walifungua ofisi na nyingine jijini Cairo, Misri.

Akiwa huko, Dk. Salim akashuhudia harakati za kujikomboa dhidi ya umangimeza wa kigeni, ZNP ikiwa katika jitihada za kujitanua namna hiyo, katika maeneo ya ughaibuni marafiki wa visiwa vya Caribbean na Kusini mwa Amerika.

Baada ya ziara fupi, anaporejea nyumbani Dk. Salim akitarajia baada ya muda mfupi angerudi tena jijini Havana, safari hii akamkuta aliyemuwezesha kufika huko, Katibu Mkuu wa ZNP, Babu, amefungwa jela.

Ikawa ngumu kwake kurejea huko, maana Babu waliyekutana kwa mara ya kwanza mwaka 1958, amekuwa muwezeshaji wa safari yake, huku akimuelimisha mengi ya kitaifa na kimataifa.

Dk. Salim, baada ya hapo mwaka 1963 akaungana na mwanahabari, pia mwanachama wa chama - ASP, wakafunga safari kwenda nchini Indonesia kuhudhuria mkutano wa wanahabari.

Baada ya kikao hicho, wakafunga safari ya nchini China, taifa linalounga mkono harakati za Kiafrika. Akiwa huko wakakutana na Waziri Mkuu, Chuo Enlai, pia viongozi wengine wa China.

Kwa Dk. Salim wakati huo, pia wengine wa ZNP kama Issa na Babu waliona mambo hayaendi sawa ndani ya chama kama yalivyokuwa matarajio yao, kuwapo mgawanyiko kutokana na matabaka na historia binafsi, wapo walioegemea fikra za utawala wa kisultani.

Wale wenye itikadi mlengo wa kushoto - Ujamaa kama vile Babu na Issa. wakajiengua mapema mwaka 1963, wakaunda chama chao cha Umma.

Katika hilo, Dk. Salim mwenyewe anaitafsiri kuwa ajali na haikupangwa. Hapo anakumbuka hata siku mbili kabla ya kutoka, akawa amechanga fedha za kuipa uhai chama chake ZNP, ikiwa sehemu ya alichopata kutoka safari yake barani Asia.

Ni baada ya miezi kadhaa tangu chama hicho cha Umma kuzaliwa, ikaunda umoja na chama cha ASP, ukiitwa 'Umoja wa Vyama vya Upizani,

Hapo ndani yake ikajumuisha chememchem kama ya vijana, kutoka umoja wa vijana wa vyama vya; ASP, Umma na Wazanzibari kwa jumla. Pia, kukawapo Chama cha Wanahabari Zanzibar; Jumuiya ya Wafanyakazi wa Zanzibar na Pemba; Umoja wa Wanafunzi Zanzibar.

Ni katika Mjumuiko huo, ukawa na Mwenyekiti Sheikh Abeid Aman Karume na Katibu Mtendaji, kijana Salim Ahmed Salim, akiwa kaiva na kupanda hadhi kitaaluma, ikiwamo 'kusafishwa macho'.

Hapo ndio kasi ya kusaka uhuru ikawa juu mnamo Desemba 10, 1963 ukapatikana uhuru 'butu' kutoka kwa Waingereza, ikiwa chini ya utawala wa Kisultani, wenye mamlaka Muungano wa vyama; ZANP na ZPPP.

ASP ikiwa katika muungano na chama cha Umma, ikayafanikisha mapinduzi ndani ya muda mfupi, kuunda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na hadi kufika Aprili 1964, Zanzibar ikaungana na Tanganyika, kuunda iliyopata uhuru mwaka 1961.

Kufikia hatua hiyo, kijana Salim, akawa kashaiva hasa, hata Rais Julius Nyerere, akatupia jicho wasifu wake kumteua balozi anayewakilisha muugano mpya, katika nchi katika nchi kama za; Misri, India na katika makao makuu ya Umoja wa Mataifa, New York Marekani.

***• Itaendelea Septemba 30***



## TANESCO yaagizwa kukamilisha miundombinu mji wa serikali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kukamilisha kwa wakati mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umeme wa chini kwenye Mji wa Serikali Mtumba mkoani Dodoma.

Alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa miundombinu hiyo ya umeme katika mji huo.

Katibu huyo alisema kuwa TANESCO wana jukumu la usimamizi wa karibu na ulazima katika kusimamia ujenzi huo wa miundombinu ya nishati ya umeme katika mji huo kwa kuwa baada ya muda mfupi ujao mahitaji yake yatakuwa makubwa kutokana na agizo la serikali ya kuzitaka ofisi zote za serikali kuhamia jijini Dodoma ifikapo Januari mosi mwakani.

Aidha, Dk. Yonazi alitaka shirika hilo kuvipa vipaumbele viwanda vya ndani kwa kununua bidhaa zinazofaa kununuliwa nchini katika viwanda hivyo.

"Mnafahamu kuwa kuna changamoto ya kiuchumi duniani kote hivyo hatuwezi kununua nje kila kitu; vitu ambavyo vinaweza kununuliwa ndani ya nchi vinunuliwe ili kupunguza upelekaji wa fedha za Tanzania nje, ni vizuri kuhusisha viwanda vya ndani ambavyo vinawezekana kutoa huduma vitoe huduma," alifafanua Dk. Yonazi

Akisisitiza kuhusiana na ubora na muonekano wa ujenzi unaendelea katika mji huo wa serikali, alisema kuwa ni muhimu kuzingatia maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya huduma nyingine, akitolea mfano miundombinu ya umeme, maji na mawasiliano.

Hivyo alitoa wito kwa kila mkandarasi kwenye eneo lake kufuata mpango kazi ambao ulikuwa umewekwa, ili kuzingatia muda wa umaliziaji wa kazi.

Naye, Mhandisi Richard Kafura wa TANESCO alisema kuwa ujenzi wa mradi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na mkandarasi DERMO Contruction Limited na hadi sasa ujenzi wa mifereji ya kupitishia miundombinu na mifumo ya umeme wa ardhini unaendelea kutekelezwa.

# Wafugaji walalamikia vitendo vya kunyanyaswa na maofisa misitu

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WAFUGAJI katika Kijiji cha Chenene Kata ya Haneti wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wamelalamikia vitendo vya unyanyasaji ambavyo wamekuwa wakifanyiwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Wamedai unyanyasaji huo umekuwa ukifanywa na watumishi wa TFS, wakati wa utekelezaji wa zoezi la kukamata mifugo inapoingia katika Hifadhi ya Misitu ya Chenene.

Walibainisha hayo jana kijijini hapo wakati wa mkutano wa hadhara ulioandaliwa na viongozi wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), ukiwa na lengo la kujenga uhusiano baina ya jamii hiyo na TFS.

Mmoja wa wafugaji hao, Baraka Loya, alisema wafugaji wamekuwa na wakati mgumu pale ambapo mifugo yao inakamatwa inapoingia katika hifadhi ya msitu huo kwakuwa watumishi wa TFS, wamekuwa wakinyanyasa wafugaji kwa kuwapiga na kuwaweka ndani.

"Naomba kuuliza sheria hizi kandamizi utekelezaji wake ukoje kwani mfugaji mifugo yake anapokwamatwa ananyanyaswa lakini pia tozo ya ng'ombe mmoja aliyeingia kwenye hifadhi anatozwa Sh. 100,000 na kuna watu wanalipa hadi Sh. milioni 10 lakini hawapewi risiti ya malipo kwa nini?" alihoji mfugaji huyo.

Aidha, alisema TFS imekuwa ikivunja haki za wanyama kutokana na kukamata mifugo na kuifungia bila kuwapa malisho wala maji kwa siku tatu.

"Mifugo hii inapokamatwa sisi wafugaji tunatakiwa kulipa lakini jambo la ajabu ni pale ambapo mifugo inashikiliwa kwa siku zaidi ya tatu bila malisho au maji, lakini pia mifugo inafungiwa na sisi wafugaji pia tunakamatwa na kufungiwa ndani sasa tutawezaje kulipa tozo hizo" alihoji.

Naye, William Underson, alisema wafugaji wa kijiji hicho wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwemo ukosefu wa maeneo ya malisho, maji pamoja na masoko ya mifugo yao.

Alisema, hivi sasa idadi ya wafugaji pamoja na mifugo inaongezeka lakini eneo la kijiji ambalo walikuwa wakilitegemea kwa malisho limechukuliwa na TFS pamoja na taasisi zingine za umma.

"Kama mnavyoona kijiji chetu ni kidogo na eneo lote limechukuliwa na TFS na taasisi zingine za serikali ikiwemo jeshi kwa hiyo hili dogo lililosalia ndiyo tunanyang'anyana wakulima humohumo na wafugaji pia wanalitazama hilo," alisema.

Kutokana na hali hiyo, waliomba TFS kuwapatia kibali ili kuingiza mifugo wakati wa masika, ambapo maeneo mengi ya malisho yanakuwa ni mashamba ya watu ili kulinda mifugo yao isife kwa kukosa malisho.

Kamishana Msaidizi Mwandamizi wa TFS, David Mng'ong'o ambaye pia ni Meneja Huduma za Sheria TFS alisema wanachokifanya wao ni kutekeleza sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili ya kulinda hifadhi hiyo ya misitu.

"Kweli kuna changamoto ambazo zipo hapa ambazo na sisi tunapaswa kukaa na watu wetu ili kuwaelekeza namna gani sheria zinapaswa kutekelezwa badala ya kutumia nguvu kunyanyasa wafugaji.

"Lakini wafugaji pia manatakiwa kutoa taarifa kwetu na chama chenu cha wafugaji kuhusu hili na kulipa tozo za mifugo lakini hampatiwi risiti ili tuweze kulifanyia kazi kwa mujibu wa sheria kwani hakuna aliye juu ya sheria na kwa mujibu wa sheria hiyo haitowezekana sisi kutoa kibali wafugaji kuingiza mifugo yao kwani mifugo ikingia humo itaharibu ikolojia,"alisema.



Katibu wa kamati ya nyanda za malisho, migogoro na watumiaji wengine wa ardhi wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Dk. Christopher Nzella, akizungumza katika mkutano wa kujadili changamoto za wafugaji wa Kijiji cha Chenene, wilayani Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Viongozi kisiasa, serikali wafundwa kuhusu uongozi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

VIONGOZI wa kisiasa na serikali wametakiwa kutambua kuwa imani ya wananchi wao haijengwi kwa kuwapatia fedha bali kwa utendaji kazi ambao unatatua kero zinazowakabili kwenye maeneo yao.

Mhadhiri kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Lukio Mrutu, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya uongozi wa kimkakati na usimamizi wa shughuli za maendeleo kwa madiwani wa viti maalum kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza yanayofanyika mkoani hapa, yakitolewa na TIA Kampasi ya Singida.

Alisema, hapa nchini kumekuwa na tabia kwa baadhi ya watu kutafuta uongozi kwa kutumia fedha jambo ambalo linakwamisha kupatikana kwa maendeleo haraka.

Mrutu alisema ili maendeleo yaweze kupatikana viongozi waache kujiingiza katika vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka au wadhifa kwa kuwa mambo hayo ndio yanafanya wananchi kutokuwa na imani na viongozi.

"Miongoni mwa nchi zenye sera nzuri na bora ni Tanzania lakini shida ipo kwenye utekelezaji, yaani watendaji hawawezi kufanya jambo hadi wasukumwe na viongozi wa ngazi za juu," alisema.

Mrutu alisema kiongozi mzuri ni yule anayesikiliza watu na sio mbabe lakini baadhi ya viongozi wamekuwa hawapendi kukosolewa na wananchi wanawaongoza jambo ambalo halina afya katika utawala wa kidemokrasia.

"Msingi wa maadili ya viongozi ni kufanya kazi kwa uaminifu, uadilifu, upole na kwa njia inayokuza imani ya wananchi katika utekelezaji wa shughuli za umma na pia kufanya maamuzi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu kwa maslahi ya umma," alisema.

Alisema uongozi wa kimkakati ni ule unaoambatana na uwezo wa kiongozi kuongoza, kusimamia, kufanya maamuzi na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mahitaji na mabadiliko ya wakati husika.

Mrutu alisema njia za kujijenga kwa kiongozi mwanamke ni kuwa na taarifa sahihi ya kile unachokizungumza kwa wale unaowaongoza, kuwa na msimamo isiyoyumba kwa kusimama kwenye ukweli na kuwashirikisha wale wanaokuzunguka hasa wataalam ili kupata uelewa wa mambo.

Naye, Diwani wa Viti Maalum kutoka Halmashuri ya Manispaa ya Temeke, Theresia Hoza akichangia mada zilizotolewa, alisema upotevu wa fedha za mapato ya ndani katika baadhi ya halmashauri unatokana na kujengwa miradi ambayo haina tija kwa halmashauri husika.





# Serikali yazuia uchimbaji madini

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

SERIKALI wilayani Songwe imesimamisha shughuli za uchimbaji madini katika Kata ya Saza kwa muda usiojulikana baada ya kubaini kuwa wachimbaji wanakiuka taratibu na sheria ikiwamo kutokuwa na leseni.

Mkuu wa wilaya ya hiyo, Solomon Itunda alitoa tangazo la kusimamisha shughuli hizo juzi kwenye mkutano na wananchi baada ya kupokea taarifa ya kamati aliyoiunda kwa ajili ya kufanya tathimini ya shughuli za uchimbaji kwenye eneo hilo.

Itunda alisema aliunda kamati hiyo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kuwa maeneo yao ya makazi yamevamiwa na wachimbaji ambao wanachimba bila kufuata taratibu na kuharisha nyumba zao.

Alisema awali Agosti 21 mwaka huu, alisitisha shughuli za uchimbaji kwa siku saba na kuunda kamati maalumu ya kufuatilia malalamiko ambayo yalikuwa yanatolewa na wananchi.

Kamati iliwahusisha wataalamu mbalimbali ambao ni kutoka katika idara tano za madini, ardhi, sheria, mazingira na ustawi wa jamii na aliwapatia hadidu rejea kwa lengo la kubaini chanzo cha mgogoro.

Alisema kutokana na wachimbaji kukiuka masharti ya uchimabji aliamua kusitisha shughuli za uchimbaji mpaka itakapobainika kuwa matatizo yaliyopo yametatuliwa na wachimbaji wamepata vibali. "Kwa mujibu wa Sheria ya Madini Kifungu 6 (1) ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa mwaka 2017, inapiga marufuku mwananchi yeyote kufanya utafiti au kuchimba madini bila leseni, sasa hapa kuna wachimbaji 19 ambao ni mmoja pekee mwenye leseni lakini na yeye ana upungufu," alisema Itunda.

Alibainisha kuwa mchimbaji akiwa na leseni ni lazima aandae Tathimini ya Athari za Mazingira (EIA) pamoja na kuwahamisha wananchi wanaoishi eneo husika kwa kuwalipa fidia ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

Alimuagiza Ofisa Madini Mkazi kushughulikia maombi ya leseni kwa wachimbaji wote waliomba ili waendelee na taratibu zingine zinazotakiwa.

"Serikali tutasimamia maridhiano kati ya wachimbaji na wananchi, ili kupisha shughuli za uchimbaji badala ya hali ilivyo ambapo uchimbaji unafanywa kwenye makazi ya watu na kutishia usalama wao, mashimo mnayoyaacha ni hatari hasa kwa watoto," alisema Itunda.

Alisema sekta hiyo katika wilaya hiyo ni moja ya vyanzo vikuu vya mapato kwa maelezo kuwa inaingiza zaidi ya Sh. bilioni 32 kwa mwaka ikiwa ni asilimia 70 ya mapato yote ya halmashauri.

Alisema pamoja na hali hiyo lakini hawawezi kuacha sekta hiyo iendeshwe kienyeji na kwamba ndio maana wameamua kusitisha shughuli hizo ili kuweka taratibu vizuri.

Hata hivyo baadhi ya wachimbaji waliiomba serikali iwaruhusu waendelee kuchimba wakati wakiendelea kushughulikia taratibu zinazotakiwa ikiwemo leseni kwa maelezo kuwa shughuli zao kuu ni uchimbaji

Mmoja wa wachimbaji hao wadogo, Kulwa Gervas alisema licha ya wao kutokuwa na leseni lakini kwa kuwa walishaanza kufanya kazi hiyo waruhusiwe kuendelea wakati taratibu nyingine zikiendelea.

Alisema wao wako tayari kufuata taratibu zote zinazohitajika endapo wataruhusiwa na wakapewa elimu sahihi kuhusu shughuli hizo.

Kwa upande wake, Amina Juma ambaye ni mmoja wa wakazi wa eneo hilo aliishukuru serikali kwa uamuzi huo na kwamba wachimbaji hao wanatakiwa kufuata taratibu ikiwemo kuwalipa fidia.

## Viongozi wa dini wahimiza kudai risiti wakati wa ununuzi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAUMINI wa dini ya kikiristo na kiislamu pamoja na wafanyabiashara Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe wameshauriwa kutoa na kudai risiti pindi wanaponunua na kuuza bidhaa zao ili kuisaidia serikali kupata kodi.

Ushauri huo umetolewa juzi na viongozi wa dini akiwemo mchungaji kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Njombe Mjini, Nelson Godiwe, ikiwa ni muendelezo wa Kampeni ya TUWAJIBIKE inayoendeshwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe.

Godiwe alisema unapodai risiti serikali itapata kodi ambayo itasaidia kuendesha ufalme wa Mungu kwa njia ya mkono wa serikali.

Kwa upande wa Padri wa Kanisa Katoliki Parokia ya Njombe, Fransisco Chengula, alisema nchi itajengwa kwa kulipa kodi hivyo kuitaka jamii kudai risiti halali pindi wanaponunua bidhaa pamoja na wafanyabiashara kujenga utamaduni wa kutoa risiti.

Ostadhi Hamis Johari ambaye ni Imamu wa Msikiti wa Airport alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha wafanyabiashara pamoja na wanunuzi kuhakikisha wanadai na kutoa risiti halali na kwa wakati.

Nao wanafunzi wa Shule ya Sekondari Njombe ambao nao walipatiwa elimu ya kulipa kodi walisema elimu waliyopatiwa imewasaidia kufahamu umuhimu wa kodi.

Meneja wa TRA, Mkoa wa Njombe, Spesioza Owure alisema kwa Mkoa wa Njombe wamepangiwa kukusanya Sh. bilioni 17 hivyo kila mwanya wa upotevu wa mapato unapaswa kuzibwa.




Baadhi ya vijana waliochaguliwa kujiunga na mafunzo ya ufundi kupitia vyuo vya Mamlaka ya Elimu ya Ufundi (VETA) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), wakiwa na furaha, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, baada ya kukabidhiwa barua za kujiunga rasmi na mafunzo hayo yanayotolewa chini ya mradi wa KCB 2jiajiri wa Benki ya KCB Tanzania wenye lengo la kuwawezesha vijana kujiajiri. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wakazi Mbeya walalamika kukosa maji siku ya tano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa baadhi ya mitaa jijini Mbeya wamelalamikia tatizo la ukosefu wa huduma ya maji kwa zaidi ya siku tano kwenye maeneo yao wakidai kuwa wanalazimika kufuata huduma hiyo umbali mrefu, huku sababu za kukatika kwa huduma hiyo zikiwa hazieleweki.

Wananchi hao wamesema hata ikitokea huduma hiyo ikapatikana inakuwa kwa muda mfupi na kwa kiwango kidogo hivyo wakaiomba serikali kutatua kero hiyo haraka.

Nipashe ilitembelea baadhi ya maeneo jijini hapa Makunguru, Nanenane, Ilomba, Ruanda na kuzungumza na wananchi ambao walisema hawajui sababu za kukatika kwa huduma hiyo mara kwa mara.

Mmoja wa wananchi hao, Asteria Mwakyusa ambaye ni mkazi wa Makunguru alisema tatizo hilo linawaathiri zaidi wanawake na watoto ambao ndio wanaohangaika kwenda kutafuta huduma hiyo maeneo ya mbali.

Alisema wakati mwingine wanalazimika kwenda kununua maji kwa watu wenye visima na kwamba maji hayo huwa yanafaa kwa kufulia na kuoga lakini siyo kwa ajili ya kunywa.

"Tunalazimika kuamka usiku kwenda kutafuta maji, tatizo hili linahatarisha hata ndoa zetu maana hili tatizo tuliondokana nalo muda mrefu lakini kwa sasa limerejea kwa kasi kubwa sana, tunaomba serikali itusaidie," alisema Asteria.

Alisema baadhi ya wanaume wenye wivu wa mapenzi huwa wanashindwa kuwaamini wake zao kwamba kweli huwa wanafuata maji na hivyo kuziweka ndoa zao matatani.

Destina Michael mkazi wa Ilomba alisema tatizo la maji ni kubwa na kwa sasa ni wiki nzima hawapati huduma hiyo na wanatumia visima kwa usaidizi.

Alisema wamekuwa wakizishangaa takwimu za serikali kwamba jiji hilo wananchi wanapata huduma kwa zaidi ya asilimia 80 wakati maeneo mengi huduma hiyo haipatikani.

Alisema maji ya kwenye visima wanayotumia wana wasiwasi kwamba wanaweza wakapata magonjwa kutokana na kutokuwa na uhakika na ubora wake.

Taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya -WSSA) hivi karibuni kupitia kwa Ofisa Uhusiano wake, Neema Staton ilieleza kuwa tatizo la kukosekana kwa huduma ya maji linasababishwa na tatizo la kukatika kwa umeme.

Alisema vyanzo vingi vya maji vinavyotumika na Jiji hilo vinatumia nishati ya umeme kusukuma maji hivyo umeme unapokatika ni lazima huduma hiyo isipatikane kwa wananchi.

"Kumekuwa na tatizo la kukosekana kwa umeme kwa nyakati tofauti katika mitambo yetu ya kusukuma maji na hata kwenye maeneo ya kuzalishia maji na hili ndilo tatizo linaloathiri uzalishaji na usambazaji maji kwa wananchi," alisema Neema.

Hata hivyo aliwaasa wananchi kuhifadhi maji wanayopata na kuyatumia kwa uangalifu wakati tatizo hilo likiendelea kushughulikiwa na kwamba wakati huduma hiyo inapopatikana wananchi wanatakiwa kuchota na kuhifadhi.

Akizungumza na umoja wa wazee wadau wa maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Mkoa, Juma Homera aliwahakikishia kuwa huduma ya maji itakuwa inapatikana kwa asilimia 100 baada ya kukamilika mradi mkubwa wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira.

Alisema mkandarasi alishasaini mkataba na anaendelea na kazi na kwamba ukikamilika utakuwa unahudumia Jiji la Mbeya na maeneo mengine zikiwezo baadhi ya wilaya za Mkoa wa Songwe.



## Wanawake watakiwa kuondoa uwoga wakati wa uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, (TAMWA-ZANZIBAR), Dk. Mzuri Issa, amewashauri wanawake na vijana kujiamini na kuondoa uwoga wakati wa kugombea nafasi za uongozi ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya uongozi kwa wanawake yaliyokuwa na lengo la kuwajengea uwezo wa kuungana pamoja na kuleta ushawishi katika maendeleo ya ajenda mbalimbali za kitaifa.

Alisema kwa sasa dunia imetambua umuhimu wa mwanamke na imeamini kwamba mwanamke ni kiongozi kutokana na maendeleo tofauti yaliyoletwa na viongozi wanawake duniani.

Mkufunzi wa masuala ya uongozi, Imelda Lulu Urrio alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wanawake kujitambua na kutambua nafasi zao ili kufikia ndoto zao katika harakati za uongozi.

"Nafasi ya wanawake kwa sasa inazidi kuongezeka kwa sababu kuna ukuaji wa elimu kwa jamii na hata watoto wa kike wenyewe wameanza kujitambua na kujielewa, tumeona baadhi ya jamii inavyowajenga watoto wa kike kujitambua na kupelekea ongezeko kubwa la viongozi wanawake," alisema.

Mratibu wa Mradi wa Kuwawezesha Wanawake kushika nafasi za Uongozi (SWILL), Maryam Ame, alisema kwa muda mrefu wanawake wameachwa nyuma katika ngazi za maamuzi.

Alisema kwa sasa wanawake watumie fursa na haki yao ya kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa ili kufikia dhamira ya 50/50 katika masuala ya uongozi.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema wamefarijika kupata mafunzo hayo wakisema yatawajenga kuwa viongozi bora na kuahidi kuwa mabalozi wazuri kwa wanawake wenzao ili kuondosha mfumo dume uliotawala katika jamii.

"Matarajio yangu baada ya mafunzo haya ni kuwa kiongozi mwenye kujiamini na nitapambana kuwa kiongozi wa ngazi za juu zaidi katika chuo changu," alieleza Hudhaimat Haji Juma, mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

# Mafunzo kwa walimu chanzo ubora wa elimu Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema uwepo wa vituo vya ubunifu wa kisayansi na mafunzo kwa walimu hasa katika masomo ya sanyasi, hisabati na kiingereza kumechangia kuimarika kwa ubora wa elimu Zanzibar.

Aliyasema hayo wakati akizindua Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Lazima Zanzibar (ZIQUE) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB).

Alisema kutokana na kasi ya uimarishaji wa miundombinu ya elimu, tatizo la uhaba wa nafasi kwa shule litamalizika.

Abdullah alisema kutokana na kasi hiyo lazima walimu kwenda sambamba na usomeshaji wa mitaala unaozingatia umahiri ili wanafunzi kufanya vizuri zaidi katika masomo yao kwa maendeleo yao, jamii na taifa.

Aidha, alisema WB kwa muda mrefu imekuwa ikisaidia kwenye maeneo mbalimbali hasa katika eneo la huduma za jamii ikiwamo miradi ya ZABEIP iligharimu Dola za Marekani milioni 42, mradi wa ZISP, Dola za Marekani milioni 35 pamoja na mradi wa ZIQUE uliotengewa Dola za Marekani milioni 50.

Alisema miradi hiyo pamoja na miradi mingine imeleta mafanikio makubwa yakiwamo kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia yaliyosababisha kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao ya taifa hasa katika masomo ya sayansi.

Aidha, alisema miradi hiyo imesaidia kufikisha huduma ya elimu katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Aidha, alisema kuwa utekelezaji wa mageuzi hayo utachangia pia ubora wa elimu inayoendana na mahitaji ya sasa ya ulimwengu, itasaidia kuwaandaa vijana katika fani mbalimbali.

Hata hivyo, alisema kuwa serikali imeweka mkazo mkubwa katika kuimarisha elimu kwa kupambana na changamoto zinazoikabili sekta ya elimu kwa kutatua changamoto zilizoikabili sekta hiyo kwa kuwajengea uwezo na ujuzi ulio sahihi vijana kwa kuwapatia taaluma mbalimbali.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Dk. Saada Mkuya, alisema wataendelea kushirikiana na sekta zote kutafuta rasilimali fedha za ndani na mashirika ya maendeleo katika kutekeleza shughuli za kiuchumi na kijamii.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Leila Muhamed Mussa, alisema wataendelea kuwaunga mkono washirika mbalimbali kwani wamekuwa wakiwawezesha kwa kila mwaka kupitia sekta ya elimu.

Aidha, aliahidi kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na kufanya kazi nao usiku na mchana ili lengo liweze kufikiwa na kusema mwaka huu kwa mara ya kwanza wanafunzi wote wamefaulu kwenda vyuo vikuu. Mwakilishi wa WB Tanzania, Nathan Balete, alisema wanaunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa sababu wanajitihada za kukuza elimu Tanzania.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Zanzibar, Khamis Abdallah Said, alisema mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano na WB na utatekelezea kwa kipindi cha miaka mitatu.

Aidha, alisema mradi huo utagharimu Dola za Marekani milioni 50 na lengo kuu ni kuona ufaulu unaengezeka na mfumo wa elimu unaweza kuzalisha wasomi waliokuwa wazuri nchini.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, ACP Richard Mchomvu, akizungumza wakati akisikiliza na kuzitatua kero mbalimbali za wananchi wa shehia za Pangawe, Kinuni, Mwembe Majogoo na Mnarani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yakiri uhaba madaktari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Zanzibar, Masoud Muhammed, amesema bado kuna tatizo la upungufu wa madaktari katika vituo vya afya na hospitali za idara maalum.

Aliyasema hayo wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Nungwi, Abdallah Abass Wadi.

Wadi alitaka kujua wizara inamkakati gani katika kuongeza nafasi za masomo kwa mwaka huu hasa katika fani ya udaktari, ili kuondokana na upungufu uliopo.

Akijibu swali hilo, alisema miongoni mwa juhudi hizo ni kuundwa kwa kamati maalum iliyoongozwa na wataalamu wa Wizara ya Afya ambayo ilitembelea hospitali na vituo vya afya vya idara maalum Unguja na Pemba.

Alisema lengo lilikuwa ni kuona uhalisia, mahitaji na kufanya tathmini ya ukubwa wa tatizo hilo na kuishauri serikali juu ya hatua muafaka za kumaliza tatizo hilo.

Alisema Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ iliomba na kupata fursa ndogo ya kuajiri wataalamu wa kada za afya 51 kwa ngazi ya shahada ya kwanza na diploma, ili kujaza nafasi za ajira zilizoachwa wazi.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imeendelea kutoa fursa za masomo kwa watumishi wa idara maalum za Zanzibar katika sekta ya afya, ambapo jumla ya watumishi 66 kwa sasa wapo masomoni Zanzibar, Tanzania Bara pamoja na nje ya nchi.

"Ni matarajio yetu kwamba watakapomaliza masomo yao wataongeza ujuzi na kuboresha huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya vya idara maalum za Zanzibar," alisema Masoud.

Alisema ofisi inaendelea kuwatumia wataalamu wa kada mbalimbali za afya wanaojitolea katika hospitali za idara maalum za Zanzibar, kwamba hadi sasa wataalamu wanaojitolea wako 163.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SOPHIA KHALFAN ATOKWETTE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S. 3914/0104** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ALFAGEMS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/PWA/KIB/1278/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HABAKUKI SIMON MGOMBELA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS KING** yenye usajili namba **MC 150 AAE.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**MKO/RB/167/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HABAKUKI SIMON MGOMBELA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS KING** yenye usajili namba **MC 156 AAE.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**MKO/RB/167/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HABAKUKI SIMON MGOMBELA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS KING** yenye usajili namba **MC 433 AWV .** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**MKO/RB/167/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMAD MGEJA** anatangaza kupotea kwa kdi ya gari aina ya **RAV 4** yenye jina la umiliki **RAMANI INVESTMENT LIMITED** yenye namba ya usajili **T 633 DEL,** CHASSIS NAMBA: **SXA110184235** na ENGINE NAMBA: **3S24677227.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/17080/2023**

## AFRI ASIAN TRADING LIMITED

**Namba ya Usajili. 110750**

Inapenda kuwatangazia rasmi wadau wake kuwa kikao cha mwisho cha kufunga Kampuni ya **AFRI ASIAN TRADING LIMITED** kitakuwa Mnamo tarehe 28-09-2023.

**asante**

## AFRI ASIAN TRADING LIMITED

**Namba ya Usajili. 110750**

Inapenda kuwatangazia rasmi wadau wake kuwa kupitia kikao cha wakurugenzi cha tarehe 15/8/2023 kampuni ya **AFRI ASIAN TRADING LIMITED** inafungwa rasmi na mwenye madai yoyote afike ofisini kuwasilisha madai yake.

**asante**

## AFRI ASIAN TRADING LIMITED

**Namba ya Usajili. 110750**

Inapenda kuwatangazia rasmi wadau wake kuwa kupitia kikao cha wakurugenzi cha tarehe 15/8/2023 cha kufungwa kwa kampuni ya AFRI ASIAN TRADING LIMITED imemteuwa Ms. Linda E. Lugano kutoka **LEMWA ATTORNEYS S.L.P 2228 TANGA kuwa Mfilisi (Liquidator)** wa Kampuni hiyo tajwa.

**asante**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**WIVINA IBRAHIM SALILA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BAJAJ BOXER** yenye usajili namba **MC 549 DDG,** CHASSIS NAMBA: **MD2B15BX0MWG92077** na ENGINE NAMBA: **JVXWMG67393.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI
TAARIFA:**PHQ/DAR/KIN/1917/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**LUKA AUGUSTINO FWALO** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 473CUT** aina ya **TVS KING,** Chassis No. **MD6M14PA3M4AA8944,** Engine No. **AK4AM43A3801,** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/DOD/BAH/3883/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALLY SALUMU,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha nne chenye index namba **P0222/0089** kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia shule ya Sekondari ya **ZANAKI CENTRE** mwaka 2003. Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa polisi: **PHQ/ KIL/MOS/2045/2023**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**AFFIDAVIT REGARDING CORRECTION OF NAMES**
**(Made under the Oath and Statutory Declaration Act. Cap 34 [R.E 2002])**

**ROZA MODESTUS SOMBE,** Adult, Female, Christian, and Resident P.O. Box 85 Mafinga, Iringa, Mufindi do hereby **SWEAR and STATES** as follows:

1. **THAT,** I am the deponent herein and thus conversant with the facts I am about to depose.
2. **THAT,** the name, **ROSE MODESTUS MHAGAMA** is also my official name and the same is appearing in my official documents like in my National Identity Card (NIDA), voting card.
3. **THAT,** both names afore mentioned above **ROZA MODESTUS SOMBE and ROSE MODESTUS MHAGAMA** identify the same person and they are all correct names ought to identify the afore mentioned person.

I, **ROZA MODESTUS SOMBE** do verify that all what is stated in paragraph 1, 2 and 3 are true to the best of my own knowledge.
**VERIFIED at NJOMBE** this 25th Day of July, 2023.

VERIFIER

SWORN and DELIVERED at NJOMBE by the said JULIAS PETRO MWALONGO who is personally known to me on this 25th day of July, 2023.

DEPONENT



BEFORE ME:
NAME: Octavian Mbunda
SIGNATURE:
ADDRESS: 244 NJOMBE
QUALIFICATION: COMMISSIONER FOR OATHS.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 65/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU AMANZI ABDALLAH LYENE wa WAJENZI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA LYENE AMANZI ABDALLAH**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16 Mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 25 Mwezi 09 Mwaka 2023.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA BOMA**
**MKOA WA MOROGORO**

**SHAURI LA MADAI/NDOA Na......54/2023**

**JINA LA MDAI: KIKUNDI CHA JIAMINI (IDDI SALUMU SEGAMBA)**

**JINA LA MDAIWA: MICHAEL THOMAS**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu za madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa MICHAEL THOMAS WA MISONGENI MTAA WA ZAHANATI Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba(Eleza hapa habari za Madai).MADAI YA PESA TSHS.397000 Kusikilizwa upande mmoja**

Kwa hiyo unatakaiwa kufika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 29 mwezi 09 mwaka 2023 saa Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili nilazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielezo vyote vinavyohusu shauri hii kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo **tarehe 22 Mwezi 09 Mwaka 2023.**

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO MJINI**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**USIMAMIZI WA MIRATHI Na......103/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HUSSEIN BINDE MIKINA WA KICHANGANI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA BINDE HUSSEIN MIKINA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5 (2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika Shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 Mwezi 9 Mwaka 2023, kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.
**ZINGATIA:**
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
Marehemu hakuacha Wosia
Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 9 mwaka 2023

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ..............KOROGWE**

**Kituo cha OLD- KOROGWE** **Mkoa ....TANGA**

**Shauri la Ndoa Na...8...2023**

**Jina la Mdai.................FLORIAN GEORGE JIDAMVA**

**Jina la Mdaiwa ..........HAPPINESS PAULO KALEMBO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa...HAPPINESS PAULO KALEMBO.........................................**
**DAR - ES SALAAM**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya .......MADAI YA TALAKA.....................................**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi Katika Mahakama hii 4/10/2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku ilivotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo 25/9/2023.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
OLD KOROGWE

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Akiri mashtaka kuwanyanyasa mbwa kingono

**AUSTRALIA,** Uingereza

RAIA wa Uingereza, Adam Britton ambaye ni mtaalamu wa wanyama amekiri mashtaka 60 yanayohusiana na ngono na wanyama na nyenzo za unyanyasaji wa watoto.

Ilielezwa kuwa mahakama ya Australia ilimsikiliza Adam Britton akijirekodi binafsi akiwatesa makumi ya mbwa, na kusababisha karibu wote kufa.

Ilibainishwa kuwa baada ya kitendo hicho alichapisha video za matukio hayo mtandaoni, ambako pia alipata nyenzo za unyanyasaji wa watoto na kwamba wakati iliposikilizwa kesi yake waendesha mashtaka wa Mahakama Kuu ya Eneo la Kaskazini waliwasilisha mashtaka dhidi yake.

Jaji Mkuu Michael Grant, alisema alikuwa na wasiwasi kusikia ukweli wa kesi hiyo kunaweza kusababisha mshtuko, kabla ya kuchukua hatua ya kuwaruhusu maofisa wa usalama na wa mahakama kuondoka mahakamani.

Waendesha mashtaka waliiambia mahakama hiyo kuwa Britton alikuwa na hasira mbaya ya kingono kwa wanyama tangu mwaka 2014. Na kwamba licha ya kuwatumia vibaya mbwa wake, aliwalaghai wamiliki wengine wa mbwa kumpa mbwa wao na kuwanyanyasa kingono.

Ilibainishwa kuwa kati ya mbwa 42 aliowadhulumu katika muda wa miezi 18 kabla ya kukamatwa kwake, 39 walikufa. **BBC**

## Uchaguzi Mali wasogezwa tena

**BAMAKO,** Mali

MSEMAJI wa serikali ya kijeshi ya Mali, Abdoulaye Maiga, amesema nchi hiyo imeahirisha tena uchaguzi wa rais ambao ulitarajiwa kurudisha taifa hilo la Afrika Magharibi kwenye demokrasia kutokana na mapinduzi ya 2020.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mjini Bamako, Maiga alisema uchaguzi wa rais uliopangwa kufanyika Februari 2024, umeahirishwa kwa sababu za kiufundi ili kuipa nafasi serikali ya mpito kupitia taarifa za uchaguzi na kuruhusu vifungu vipya vya katiba ambavyo vinaweza kuchelewesha uchaguzi huo.

Inaelezwa kuwa ni mara ya pili kwa serekali ya kimapinduzi ya Mali ambayo imetokana na mapinduzi mawili mwaka 2020 kuahirisha uchaguzi wa rais wa nchi.

Wanasiasa wa Mali wamekosoa uamuzi huo ambao unaweza kusababisha vikwazo vya kiuchumi kwa Mali kutoka Jumuiya ya Mataifa ya Magharibi (ECOWAS).

Jumuiya hiyo ililegeza vikwazo kwa Mali Julai 2022 baada ya serikali kuahidi kufanya uchaguzi. **VOA**

# Mashambulizi nchini Yemen yahatarisha juhudi za amani

**SANA'A,** Yemen

WAASI wa Houthi na muungano unaoongozwa na Saudi Arabia, wametuhumiana kwa mashambulizi yanayovunja hali ya utulivu na kuhatarisha mazungumzo ya amani.

Mapambano yanayojitokeza nchini Yemen yanatekelezwa na pande mbili na yanatajwa kudumu nchini humo tangu 2005, katika mzozo ambao umesababisha vifo vya maelfu ya watu na kuwaacha asilimia 80 ya wakazi wakitegemea msaada.

Msemaji wa Wahouthi Mohammed Abdulsalam, alisema muungano huo uliwaua wanajeshi wake 12 mwezi uliopita kwenye eneo la mpaka na Saudi Arabia.

Waasi wa Houthi wanaoungwa mkono na Iran walikuwa wakijibu tuhuma za kuwaua wanajeshi wawili wa Bahrain na kuwajeruhi wengine kadhaa jana kwenye shambulizi la ndege isiyo na rubani katika mpaka wa kusini mwa Saudi Arabia.

**Televisheni ya Wahouthi ya Al-Masirah iliripoti kwamba raia wanne walijeruhiwa katika mashambulizi ya Saudi Arabia katika himaya ya Yemen karibu na mpakani.**

Muungano unaoongozwa na Saudi Arabia umelaani mauaji hayo na kusema yalifuatia mashambulizi kadhaa ya Wahouthi kwenye kituo cha kusambaza umeme na kituo cha jeshi la polisi karibu na mpakani.

Kamandi ya jeshi la Bahrain, ilisema mmoja wa maofisa wake pamoja na mwanajeshi mmoja waliuliwa kwenye shambulizi la ndege isiyo na rubani na waasi wa Yemen waliokuwa wanapiga doria katika mpaka kati ya Yemen na Saudi Arabia.

Taarifa ya jeshi la Bahrain iliyoripotiwa na shirika rasmi la habari la Bahrain, ilisema wanajeshi kadhaa walijeruhiwa katika shambulio hilo.

Taarifa hiyo ya jeshi pia ilisema shambulizi hilo la kigaidi lilifanywa na waasi wa Houthi ambao walitumia ndege isiyo na rubani kulilenga eneo la walinzi wa Bahrain katika mpaka wa kusini na ufalme wa Saudi Arabia licha ya kusitishwa kwa operesheni za kijeshi kati ya pande zinazohasimiana nchini Yemen.

Pia Saudi Arabia ililaani shambulizi hilo katika himaya yake lililowaua wanajeshi wawili wa Bahrain karibu na mpaka wake na Yemen. Huku Wizara ya Mambo ya Nje ya Saudi Arabia ikitoa taarifa ya kulaani na kushutumu kile ilichokieleza kuwa ni shambulizi la kihaini dhidi ya Ufalme wa Bahrain upande wa mpaka wa kusini, ambalo lilisababisha kuuliwa kwa wanajeshi wake kadhaa na wengine kujeruhiwa.

Taarifa ya Saudi Arabia haikuwalaumu moja kwa moja waasi wa Houthi wanaoungwa mkono na Iran, lakini ikarudia wito wa ufalme huo kutaka usafirishaji na upelekaji silaha kwa wahouthi ukome. Wahouthi hawajatoa kauli yoyote kuhusu shambulizi hilo.

Televisheni ya Wahouthi ya Al-Masirah iliripoti kwamba raia wanne walijeruhiwa katika mashambulizi ya Saudi Arabia katika himaya ya Yemen karibu na mpakani.

Shambulizi lililowaua wanajeshi wa Bahrain limefanyika wakati Saudi Arabia ikifanya juhudi kutafuta usitishwaji mapigano wa kudumu, karibu mwaka mmoja na nusu baada ya makubaliano ya kusitisha mapigano na Wahouthi ambayo kwa kiwango kikubwa yameheshimiwa licha ya kufikia mwisho rasmi mwezi Oktoba 2022. **DW**



Wakazi wa mji wa Mushaki, Goma nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wakirejea katika makazi yao baada ya waasi wa M23 kuanza kuondoka kwenye eneo hilo, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Waziri wa Iran akataliwa kuingia Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imekataa maombi ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, ya kutembelea Washington, wiki iliyopita sababu ikiwa ni wasiwasi wa rekodi ya Tehran ikijumuisha kushikiliwa kwa raia wa Marekani siku za nyuma.

Waziri huyo wa Iran Hossein Amir-Abdollajian, aliripotiwa kutaka kusafiri kutembelea ofisi ya ubalozi baada ya baraza kuu la Umoja wa Mataifa jijini New York.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Matthew Miller, aliwaambia wanahabari kwamba waliwasilisha maombi yake lakini yalikataliwa na wizara.

Alisema kwamba hawana jukumu la kuruhusu maofisa wa Iran na mataifa mengine wa serikali kusafiri kwenda New York kwa shughuli za Umoja wa Mataifa, lakini linapokuja suala la kuja Washington, jukumu hilo ni la kwao.

Iran wiki iliyopita iliwaachilia raia watano wa Marekani kutoka gerezani kwa kubadilishana na kuachiliwa dola bilioni sita za Iran kutoka Korea Kusini katika akaunti yake ya Qatar. **VOA**

# SINGIDA FG YAPAA MISRI IKIJIPA SAA 72 KUPIKA DOZI YA FUTURE

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Singida Fountain Gate, limesema lina saa 72 za kufanya mazoezi wakiwa nchini Misri ambayo yatawasaidia kuifunga timu ya Future FC Jumapili katika mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho barani Afrika kuwania kufuzu hatua ya makundi.

Singida FG Jumapili itashuka katika Uwanja wa Al Salam, Cairo nchini Misri ikiwa na mtaji wa bao 1-0 iliyoupata hapa nchini kwenye mechi ya awali iliyopigwa Dimba la Azam Complex, Dar es Salaam, shukrani kwa Elvis Rupia, waliyemsajili msimu huu akitokea Polisi ya Kenya.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana mchana kabla ya kuanza safari kuelekea Misri, Mkurugenzi wa Ufundi wa timu hiyo, Ramadhan Nsanzurwimo, alisema siku hizo zitawasaidia kwa kiasi kikubwa wachezaji wao kuhakikisha wanaingia hatua ya makundi.**

"Tuna saa 72 ambazo zitatutosha kufanya maandalizi ya mwisho tukiwa Misri kuelekea kwenye mchezo wetu huo, kila mchezaji ana morali ya juu," alisema Nsanzurwimo.

Alisema wamefanya maandalizi ya kutosha jijini Dar es Salaam katika kipindi chote walichokuwa wameweka kambi yao baada ya kumaliza mchezo wao wa awali ambao walifanikiwa kushinda bao 1-0.

Katika hatua nyingine Msemaji wa timu hiyo, Hussein Masanza, alisema wameondoka na kikosi cha wachezaji 21 ambao anaamnini watakwenda kutoa ushindani katika mchezo huo huku wakiwaacha baadhi ya nyota wengine akiwamo Joash Onyango, Abdul Majid Mangalo na Frank Mkumbo.

Aliwataka Watanzania waendelee kuwaombea ili watimize malengo yao kwani mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu kwa kuwa watakuwa ugenini.

"Tunaomba Watanzania mtuombee kwani mchezo wa ugenini huwa mgumu, tunafahamu Waarabu wakiwa nyumbani kwao wanafanya kila njia ili kumharibia mchezo mpinzani wake," alisema Massanza.

Matokeo ya sare yoyote ama ushindi, yataifanya Singida FG kutinga hatua ya makundi na kuweka rekodi kwa kuwa timu ya kwanza kutoka Tanzania kupanda daraja na kutinga hatua hiyo kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

## *Twiga Stars yasonga mbele WAFCON*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Soka ya Tanzania ya Wanawake, Twiga Stars, imefanikiwa kusonga mbele katika kampeni yake ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika (WAFCON) zitakazofanyika mwakani nchini Morocco baada ya kuisukumiza nje Ivory Coast kwa mikwaju 4-2 ya penalti.

Katika mechi hiyo iliyopigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam jana, penalti za Twiga Stars ziliwekwa ndani ya kamba na Ester Mabanza, Anastazia Katunzi, Denisia Minja na Opa Clement, Ezekia Kasonga akikosa mkwaju wake baada ya kuokolewa na kipa Aminata Diabate.

Penalti za Timu ya Taifa ya Ivory Coast zilifungwa na Mariam Diakite na Rebecca Ida, huku Bernadette Amani na Mariam Sidibe wakikosa mikwaju yao iliyopanguliwa kwa ustadi na kipa Najat Abbas.

Timu hizo zililazimika kupigiana penalti baada ya dakika 90 kumalizika Twiga Stars ikiwa mbele kwa mabao 2-0 katika mechi ya jana, lakini Ijumaa iliyopita nchini Ivory Coast, Tanzania ilifungwa mabao 2-0, hivyo matokeo ya jumla yalikuwa ni 2-2.

Kwa matokeo hayo, Twiga Stars huenda ikakutana na Timu ya Taifa ya Togo ambayo nayo ina mechi ya marudiano dhidi ya timu kibonde ya Djibouti iliyofungwa mabao 7-0 mchezo wa awali. Timu itakayoibuka mshindi katika raundi hiyo inayofuata kati ya Twiga Stars na Togo vs Djibouti, itafuzu kucheza fainali hizo hapo mwakani.

Mabao ya dakika 90 za mchezo ya Twiga yalifungwa na Minja dakika ya 49 kwa faulo ya moja kwa moja kwa mguu wa kushoto, kabla ya Opa kupachika bao la pili dakika mbili baadaye akimalizia pasi ya kifua kutoka kwa mfungaji wa bao la kwanza Minja.

Bao hilo lilitokana na faulo iliyopigwa na Anastazia na kuzua kizaazaa kwenye lango la Ivory Coast na Minja alimsukumia Opa ambaye naye alipachika kwa mguu wa kushoto. Mechi ilianza kwa wageni kufanya mashambulizi makali langoni mwa Twiga Stars ikiwatumia mawinga wao wenye kasi, lakini uhodari wa kipa Najat Abbas uliwanyima mabao dakika ya 11, 15 na 38, ambapo wachezaji Rosemonde Kouassi na Mariam Diakite walifanya majaribio ya hatari.

Katika dakika 45 za kwanza, wachezaji wa Twiga Stars walionekana kupoteza mipira iliyoshia kwenye miguu ya wachezaji wa Ivory Coast.

Ni kipindi ambacho wageni walionekana kucheza kwa kutulia zaidi na kumiliki mpira kutokana na kuwa na mtaji wa mabao 2-0 waliloupata nyumbani Ijumaa iliyopita. Twiga Stars ilianza kufanya shambulizi la kwanza la hatari dakika ya 40, wakati Opa alipopiga krosi iliyopanguliwa na kipa Aminata na kumkuta Amina Bilal akiwa kwenye nafasi nzuri, huku kipa wa Ivory Coast na beki wake wakiwa wamegongana na kuanguka chini, lakini alipiga shuti lililopaa juu la lango.



Mshambuliaji wa Simba, Shaban Chilunda, akibinjuka kucheza mpira wakati wa mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, kujiandaa na mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia Jumapili wiki hii. **PICHA: SIMBA**

## KMKM, KVZ, zachuana kileleni Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MZUNGUKO wa tatu wa Ligi Kuu Zanzibar umemalizika huku KMKM ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa baada ya kulingana pointi saba sawa na KVZ na JKU SC.

Katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 16, KMKM SC imefanikiwa kukaa kileleni mwa ligi hiyo baada ya kushinda mchezo wake wa tatu kwa bao 1-0 dhidi ya wenyeji wao, Maendeleo FC uliopigwa Kisiwani Pemba.

Kwa upande wa KVZ, yenyewe mchezo wake wa tatu imetoka suluhu dhidi ya Mlandege FC, na katika msimamo nafasi ya tatu ikishikiliwa na JKU SC ambayo nayo inazidiwa kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa na miamba hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu huu imekuwa tofauti na misimu iliyopita kutokana na ushindani kuongezeka.

Alisema kila timu inayoshuka nayo dimbani inacheza tofauti na ilivyokuwa ikicheza hapo awali, jambo linalosababisha kama kocha kuchukua maamuzi ya haraka kulingana na mabadiliko ya mchezo wakati unaendelea uwanjani.

"Ligi Kuu msimu huu imeanza kwa kasi ya ajabu, katika michezo mitatu tuliyocheza yote ni migumu mno, hizi timu zilizopanda daraja pia zina wachezaji ambao wanasumbua uwanjani hali inayosababisha hata ukipata alama tatu basi kikosi chako kiwe kimefanya kazi kubwa kweli," alisema.

Ligi Kuu ya Zanzibar mzunguko wa nne itaendelea tena leo Jumatano kwa kuchezwa mchezo mmoja utakaopigwa Finya, Kisiwani Pemba ukizikutanisha Ngome FC na wenyeji wao, Maendeleo FC.

Ngome FC inashuka dimbani ikiwa na alama mbili katika nafasi ya 12 huku wenyeji wao hao, Maendeleo FC wakiwa na alama moja na nafasi ya pili kutoka mkiani kwenye ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

**Kila timu inayoshuka nayo dimbani inacheza tofauti na ilivyokuwa ikicheza hapo awali, jambo linalosababisha kama kocha kuchukua maamuzi ya haraka kulingana na mabadiliko ya mchezo wakati unaendelea uwanjani.**

## ZISIKUPITE

### WAJITOSA KWA TONEY

ARSENAL wako tayari kuongeza nia ya kumnunua mshambuliaji wa England, Ivan Toney katika dirisha la Januari, huku Brentford wakimpa thamani ya pauni milioni 60 mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Mirror)***

### PAVLIDIS AWINDWA

KLABU ya Brentford inafikiria kusajili mshambuliaji mpya huku mchezaji wa Wolfsburg, Jonas Wind, 24, mshambuliaji wa AZ Alkmaar na Ugiriki, Vangelis Pavlidis na mchezaji wa Kimataifa wa Brazil na Santos, Marcos Leonardo, 20, wako kwenye orodha yao fupi. ***(90min)***

### LUKAKU MKATABA MPYA

AS Roma ina nia ya kubadilisha mkopo wa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku kutoka Chelsea kuwa mkataba wa kudumu na wanaweza kumpa mshambuliaji wa England, Tammy Abraham, 25, kuwa sehemu ya kubadilishana. ***(Calciomercatoweb)***

### CHELSEA YATEMA KOCHA

CHELSEA imeachana kwa siri na Bruno Saltor, ambaye alijiunga na benchi la kocha wa zamani, Graham Potter na alikuwa kocha wa kikosi cha kwanza chini ya kocha mpya, Mauricio Pochettino. ***(Telegraph)***

### DAVIES ATAJWA MADRDID

REAL Madrid pia wana nia ya kumsajili beki wa kushoto wa Canada, Alphonso Davies, 22, kutoka Bayern Munich. ***(Football Transfers)***

### MAROTTA MKATABA MPYA

MTENDAJI Mkuu wa Inter Milan, Beppe Marotta, amesema klabu hiyo hivi karibuni itakutana na mlinzi wa Italia, Federico Dimarco, 25, kujadili mkataba mpya. ***(Radio Anch'Io Sport, via Gazzetta dello Sport)***

### TOMORI AFUNGUKA YA PSG

MLINZI wa England, Fikayo Tomori, 25, alikataa ombi la Paris St-Germain msimu wa majira ya joto ili kusalia AC Milan. ***(Calciomercato)***

### LINGARD BASI TENA

KLABU ya West Ham imeachana na mpango wa kumsajili winga wa England, Jesse Lingard, 30, kwa uhamisho huru, huku mchezaji huyo akifanya mazoezi na Al Ettifaq. ***(Mail)***

### UEFA YASHUTUMIWA

SHIRIKISHO la soka la Ulaya, Uefa limeshutumiwa kwa kuwasilisha ushahidi "usio wa kweli" kwa uchunguzi wake huru kuhusu machafuko kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2022 kati ya Liverpool na Real Madrid mjini Paris. ***(Guardian)***


### HAG, SANCHO KUSULUHISHWA

CHAMA cha Wanasoka wa Kulipwa (PFA), kimejitolea kusaidia katika jitihada za kuwasaidia Erik Ten Hag na Jadon Sancho ili kumaliza tofauti zao. ***(Times)***

### RODRYGO ANUKIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inavutiwa na winga wa Real Madrid na Brazil, Rodrygo, 22, ili kukabiliana na miamba hiyo ya Hispania inayomsaka fowadi wao wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 24. ***(Football Transfers)***

## DONDO SOKA
## MAGAZE ULAYA




# SANCHO ATAKIWA KUMWOMBA MSAMAHA KOCHA TEN HAG

**MANCHESTER,** England

● ● ● Afukuzwa maeneo yote ya kikosi cha kwanza hadi kantini, Rashford, Shaw na Maguire...

JADON Sancho ameshauriwa kumwomba msamaha Kocha Erik ten Hag na wachezaji wenzake wa Manchester United, kwa mujibu wa ESPN.

**Sancho amefukuzwa kwenye mazoezi ya kikosi cha kwanza baada ya mzozo wake na Ten Hag kwa kuachwa nje ya kikosi kwa ajili ya mechi ya United dhidi ya Arsenal mapema Septemba.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hadi sasa amekataa kuomba msamaha na ameondolewa kikosini.

Mpambano huo umedumu kwa zaidi ya wiki tatu na wachezaji wenzake Sancho, wakiongozwa na Marcus Rashford, Luke Shaw na Harry Maguire, wamejitokeza kusuluhisha hali hiyo.

Sancho, kwa mujibu wa chanzo, ameambiwa na wachezaji wenzake wa England kumuomba msamaha Ten Hag ili kuokoa maisha yake pale Old Trafford.

Mshambuliaji huyo wa England, hajazingatiwa kuchaguliwa kwa mechi dhidi ya Brighton, Bayern Munich na Burnley huku akibakia nje ya kikosi cha kwanza kwenye mazoezi.

Pia amefukuzwa kutoka maeneo yote ya kikosi cha kwanza ikiwa ni pamoja na vyumba vya kubadilishia nguo na kantini.

Sancho kwa sasa anafanya mazoezi peke yake kwenye viwanja vya akademi na haruhusiwi kujitosa kwa wachezaji wenzake.

Chama cha Wanasoka wa Kulipwa (PFA), kinafanyia kazi tatizo hilo ili kuwapatanisha Sancho na Ten Hag na kutafuta njia ya kujenga upya uhusiano wao.

Sancho yuko tayari kuondoka katika klabu hiyo katika dirisha la usajili la Januari, lakini bado ana mkataba hadi mwaka 2026.

Aliwasili United kutoka Borussia Dortmund kwa ada ya pauni milioni 73 mwaka 2021.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,157,2

MECHI KALI
BRENTFORD
VERSUS
ARSENAL
1|3.13
X|3.43
2|2.11

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Abbas Hussein - 0655 277 XXX
2. Mada Mawinda - 0657 695 XXX
3. Iddi Amri - 0658 771 XXX
4. Bazili Ngede - 0677 671 XXX
5. Miraji Ramadhan - 0678 885 XXX
6. Agnes Sijaona - 0711 263 XXX
7. Asha Nassoro - 0711 400 XXX
8. Safael Mpolo - 0713 588 XXX
9. Lusia Mlulu - 0715 585 XXX
10. Aliasi Chogogwe - 0715 874 XXX
20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RICE, TROSSARD HAWANA MAJERAHA MAKUBWA




**LONDON,** England

ARSENAL ina uhakika wa kuepuka janga la majeruhi baada ya vipimo vya awali vya Declan Rice na Leandro Trossard kuonesha hawajaumia sana, kwa mujibu wa ESPN.

Rice alitolewa wakati wa mapumziko katika sare ya mabao 2-2 na Tottenham Hotspur Jumapili kutokana na kile kocha Mikel Arteta alichoeleza baadaye kama "maumivu mgongoni mwake."

Kiungo huyo alisema kuwa bado anatatizwa na tatizo hilo lakini sio kwa ukubwa sana. Vilevile, Trossard alikosa kabisa mchezo baada ya kupata jeraha la misuli ya paja, lakini anatarajiwa kurejea mazoezini baadaye wiki hii.

Ingawa wote wawili wana uwezekano wa kutocheza mechi ya leo Jumatano ya Kombe la EFL ya mzunguko wa tatu dhidi ya Brentford. Trossard hana nafasi ya kuwa kwenye safari ya Jumamosi ya Ligi Kuu dhidi ya Bournemouth.

Haijulikani ni lini Rice atarejea lakini kutokuwapo kwake kutakuwa kwa muda mfupi. Bukayo Saka alionekana akichechemea mwishoni mwa mchezo wa Jumapili, lakini vyanzo vilisema hatarajiwi kuwa nje kwa muda mrefu.

Naye, Gabriel Martinelli anaendelea kupata nafuu kutokana na jeraha la misuli ya paja na huenda akarejea ndani ya wiki mbili zijazo.

Thomas Partey ana matumaini ya kuwa sawa kuelekea kwenye mchezo dhidi ya Manchester City kule Emirates Jumapili wiki hii, ingawa hakuna uhakika wa hilo kwa wakati huu.



# Enrique aondoa hofu kwa Mbapp

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Luis Enrique, amepuuza wasiwasi kuhusu Kylian Mbappe baada ya mshambuliaji huyo wa Ufaransa kutolewa nje katika ushindi wao wa mabao 4-0 dhidi ya Marseille.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, hakuweza kuendelea kucheza baada ya kutibiwa tatizo la kifundo cha mguu mapema kwenye mechi hiyo.

Baada ya mchezo huo, kocha huyo raia wa Hispania alidai kumtoa ilikuwa ni sehemu tu ya tahadhari.

Alisema: "Sijui ni nini hasa kilitokea, lakini nadhani aliumia kidogo. Alijaribu kuendelea lakini bado alikuwa na maumivu.

"Sidhani kama jambo hilo ni zito na nadhani atarejea hivi karibuni lakini ni bora kuchukua tohadhari.

Licha ya kukosekana kwa Mbappe, mabingwa hao watetezi wa Ligue 1 hawakupata taabu kuwachabanga Marseille 4-0.

Achraf Hakimi alianza kuifungia PSG kwa mkwaju wa faulo kabla ya Randal Kolo Muani kufunga bao lake la kwanza kwa klabu hiyo.

Kipindi cha pili, Go
Ramos alifunga kwa pa
Ousmane Dembele na
kuongeza jingine kwa asi
kolo Muani.

Mshambuliaji huyo
Ureno alifurahi kupata m
yake ya kwanza kwa
hiyo lakini akataka kuan
mechi inayofuata.

Alisema: "Nina furaha
sababu ni ushindi mk
dhidi ya timu nzuri na
furaha kwa sababu hati
niliweza kufunga.

"Ni maalum, ni sawa ku
hia sasa ushindi, lakini
ni siku mpya, kwa hivyo la
tuzingatie mchezo unaof

90,273/-

# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/09/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Liverpool FC | 2.80 | 3.90 | 2.15 |
| 02. 30/09/23 | 20:00 | Boavista Porto vs FC Famalicao | 2.17 | 3.30 | 3.15 |
| 03. 30/09/23 | 22:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.21 | 3.15 | 3.25 |
| 04. 30/09/23 | 22:00 | AS Monaco vs Olympique Marseille | 2.20 | 3.65 | 2.85 |
| 05. 01/10/23 | 13:30 | Fatih Karagumruk Istanbul vs Kasimpasa Istanbul | 2.28 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 01/10/23 | 14:30 | FC Nuremberg vs FC Magdeburg | 2.37 | 3.55 | 2.65 |
| 07. 01/10/23 | 14:30 | SV 07 Elversberg vs Greuther Furth | 2.50 | 3.60 | 2.48 |
| 08. 01/10/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Kaiserslautern | 2.65 | 3.45 | 2.42 |
| 09. 01/10/23 | 16:00 | Nottingham Forest vs Brentford FC | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 10. 01/10/23 | 16:00 | Udinese Calcio vs Genoa CFC | 2.08 | 3.20 | 3.45 |
| 11. 01/10/23 | 17:15 | Deportivo Alaves vs CA Osasuna | 2.55 | 3.00 | 2.80 |
| 12. 01/10/23 | 17:30 | FC Luzern vs FC Zurich | 2.24 | 3.25 | 2.70 |
| 13. 01/10/23 | 18:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.33 | 3.35 | 2.55 |
| 14. 01/10/23 | 18:00 | Hobro IK vs Kolding IF | 2.65 | 3.25 | 2.31 |
| 15. 01/10/23 | 19:00 | Konyaspor vs Besiktas Istanbul | 2.80 | 3.30 | 2.19 |
| 16. 01/10/23 | 19:00 | Viborg FF vs AGF Aarhus | 2.60 | 3.35 | 2.50 |
| 17. 01/10/23 | 19:00 | Atalanta BC vs Juventus Turin | 2.46 | 3.30 | 2.70 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 27/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1820 | Enppi Club vs Talaea El Gaish | 2.68 | 2.83 | 2.78 |
| 18:30 | 5926 | NK Celje vs NK Aluminij | 1.30 | 4.85 | 7.28 |
| 19:00 | 4365 | Al Hidd Club vs Riffa Club | 5.71 | 4.03 | 1.48 |
| 19:30 | 4487 | Cagliari vs AC Milan | 4.92 | 3.69 | 1.74 |
| 19:30 | 5487 | Verona vs Atalanta | 4.22 | 3.70 | 1.84 |
| 19:30 | 5915 | Empoli vs Salernitana | 2.33 | 3.30 | 3.15 |
| 19:45 | 2201 | PSV Eindhoven vs GO Ahead Eagles | 1.14 | 7.34 | 12.90 |
| 20:00 | 1390 | Athletic Bilbao vs Getafe | 1.64 | 3.66 | 5.98 |
| 20:00 | 1759 | Osters IF vs Helsingborg | 1.46 | 4.39 | 6.27 |
| 20:00 | 2781 | Borussia Dortmund II vs Duisburg | 2.02 | 3.67 | 3.21 |
| 20:00 | 2812 | Maccabi Haifa vs Bnei Sakhnin | 1.20 | 5.86 | 9.29 |
| 20:00 | 3147 | Real Madrid vs Las Palmas UD | 1.28 | 5.76 | 10.21 |
| 20:00 | 3582 | Ostersunds vs IK Brage | 2.25 | 3.39 | 3.03 |
| 20:00 | 4022 | Adana Demirspor vs Besiktas | 3.15 | 3.66 | 2.02 |
| 20:00 | 4882 | Villarreal vs Girona | 2.28 | 3.64 | 2.97 |
| 20:30 | 3477 | Mamelodi Sundowns vs Stellenbosch | 1.41 | 4.02 | 7.66 |
| 20:30 | 4116 | Olympiakos vs Aris Salonica | 1.41 | 4.11 | 8.33 |
| 20:30 | 5211 | PAOK vs Volos | 1.21 | 6.25 | 11.46 |
| 20:30 | 5738 | Kaizer Chiefs vs Sekhukhune United | 1.89 | 3.14 | 4.11 |
| 21:00 | 1455 | Sporting Farense vs Tondela | 1.75 | 3.62 | 4.51 |
| 21:00 | 2624 | Pogon Szczecin vs Legia Warszawa | 2.44 | 3.28 | 2.52 |
| 21:00 | 3527 | Al Kuwait SC vs Al Salmiyah | 1.53 | 4.35 | 4.45 |
| 21:00 | 4062 | Twente vs Vitesse Arnhem | 1.37 | 4.76 | 6.74 |
| 21:15 | 1854 | Domzale vs NK Mura | 2.11 | 3.27 | 3.02 |
| 21:30 | 1163 | Como vs Sampdoria | 2.37 | 3.19 | 2.83 |
| 21:30 | 2123 | FC Lugano vs Lausanne-Sport | 1.87 | 3.60 | 3.65 |
| 21:30 | 4142 | Parma vs Bari | 1.93 | 3.24 | 3.80 |
| 21:30 | 4198 | Catanzaro vs Cittadella | 2.17 | 3.13 | 3.23 |
| 21:30 | 5019 | Servette Geneva vs FC Winterthur | 1.73 | 3.77 | 4.13 |
| 21:30 | 5908 | St. Gallen vs BSC Young Boys | 2.49 | 3.55 | 2.48 |
| 21:45 | 1520 | Chelsea vs Brighton | 2.42 | 3.45 | 2.62 |
| 21:45 | 1550 | Lazio vs Torino | 2.19 | 3.29 | 3.45 |
| 21:45 | 1763 | Hibernian vs St Mirren | 2.13 | 3.25 | 3.10 |
| 21:45 | 1824 | Aston Villa vs Everton | 1.70 | 3.82 | 4.27 |
| 21:45 | 2075 | Liverpool vs Leicester | 1.46 | 4.48 | 5.60 |
| 21:45 | 2149 | Lincoln vs West Ham | 6.69 | 4.46 | 1.41 |
| 21:45 | 2186 | Royal Antwerp vs KAA Gent | 2.10 | 3.57 | 3.03 |
| 21:45 | 2652 | Bournemouth vs Stoke City | 1.60 | 3.94 | 4.89 |
| 21:45 | 3737 | Napoli vs Udinese | 1.45 | 4.61 | 6.91 |
| 21:45 | 4087 | Fulham vs Norwich City | 1.54 | 4.09 | 5.18 |
| 21:45 | 4249 | Inter vs Sassuolo | 1.40 | 5.13 | 7.03 |
| 21:45 | 4526 | Blackburn vs Cardiff | 1.95 | 3.54 | 3.44 |
| 21:45 | 5051 | Ross County vs Aberdeen | 2.55 | 3.11 | 2.60 |
| 21:45 | 5423 | Brentford vs Arsenal | 3.13 | 3.43 | 2.11 |
| 21:45 | 5982 | Wehen vs RB Leipzig | 14.78 | 7.60 | 1.16 |
| 22:00 | 5454 | Rangers vs Livingston | 1.13 | 6.71 | 15.26 |
| 22:00 | 5931 | Newcastle vs Manchester City | 2.62 | 3.40 | 2.44 |
| 22:30 | 1867 | Valencia vs Real Sociedad | 2.62 | 3.13 | 2.87 |
| 22:30 | 4507 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.52 | 3.19 | 2.94 |
| 22:45 | 1435 | Leixoes vs GD Estoril | 3.04 | 3.20 | 2.34 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# HATIMA YA TANZANIA, KENYA, UGANDA KUANDAA AFCON 2027 KUJULIKANA LEO

**Na Adam Fungamwango**

HATIMA ya nchi za Afrika Mashariki, Tanzania, Kenya na Uganda kuandaa Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, itajulikana leo jijini Cairo, Misri.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), leo linatarajiwa kutatangaza nchi zilizoshinda maombi hayo baada ya kupigiwa kura na wajumbe, huku nchi hizo za Afrika Mashariki zikiwa moja kati ya zilizoomba kuandaa kwa pamoja.

Viongozi wa soka Tanzania wakiongozwa na rais Wallace Karia wapo jijini Cairo kushuhudia upingwaji wa kura na utangazaji, ambapo serikali inaongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro.

**Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo, alisema hata wakati wanaomba walijua watapata upinzani kutoka mataifa mengine ambayo nayo yaliomba.**

"Tuliomba na tulijua tuna upinzani kutoka mataifa mengine mbalimbali, kwa hiyo kama uliomba inamaana lazima uamini unaweza kupata na kuandaa, ndivyo tunavyoamini sisi," alisema.

Alisema anaamini kampeni iliyopigwa kwa wajumbe mbalimbali inaweza kufanikisha kile walichoomba.

"Kwa sasa Ujumbe wa Tanzania upo Cairo nchini Misri ukiongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, lakini rais wa TFF yupo huko na wengine wengi ambao watahudhuria mkutano huo, ni ujumbe mzito uliokwenda, lakini kesho (leo), ndiyo itakwenda kufahamika nini ambacho kitatokea kwetu.

"Nia yetu ni kuandaa fainali za AFCON 2027 pamoja na wenzetu Kenya na Uganda, sisi bado tunaamini kuwa nafasi hiyo ipo, lakini tusubiri tuone baada ya kutangazwa nani atakuwa mwenyeji," alisema.

Siku chache kabla ya kuteuliwa kuwa Balozi, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Said Yakubu, baada ya kikao na makatibu wakuu wenzake kutoka Kenya na Uganda, alisema walikuwa wamejipanga kuwahi nchini Misri kwa ajili ya kuanza kampeni zitakazowashawishi wajumbe wawapigie kwa ajili ya kupata kura zao, huku pia wakitumia njia za kidiplomasia pamoja na kuwatumia viongozi wenye ushawishi kama rais Karia pamoja na Leodgar Tenga ili kuwafikia wajumbe.

## Inonga kurejea

INATOKA UK. 24

"Kramo alipata matatizo ya goti siku 20 zilizopita na yeye anaendelea na matibabu vizuri kabisa, kuna hatua tukifika ndiyo tutajua ni lini atarejea uwanjani ila kwa sasa bado tupo katika hatua ya mwanzo ya matibabu," alibainisha daktari huyo.

Katika mechi yake ya kirafiki kabla ya kuivaa Power Dynamos ya Zambia, Oktoba Mosi Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam katika mechi ya mkondo ya pili Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba jana asubuhi, iliirarua Pan African inayocheza Ligi ya Championship mabao 4-0.

Mabao ya Simba yaliwekwa nyavuni na Saido Ntibazonkiza, Moses Phiri, Kibu Denis na Willy Onana.

Wakati huo huo, timu ya Power Dynamos imeelezwa inaweza kumkosa kipa wake namba moja, Lawrence Mulenga, katika mechi ya marudiano dhidi ya Simba Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Kipa huyo aliyeokoa hatari nyingi na kuinyima Simba ushindi wa ugenini aliumia katika mechi ya Ligi Kuu ya Zambia dhidi ya Zesco na kukimbizwa hospitalini, mchezo huo ukimalizika kwa sare ya mabao 2-2 kama ilivyokuwa katika matokeo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



Gamondi

## Gamondi kuishangaza

INATOKA UKURASA 24

Kwa mujibu wa Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, hali ya kambi iko vizuri na wachezaji wote wako salama kwa ajili ya maandalizi ya mechi yao dhidi ya Al-Merrikh.

"Tuna mechi ngumu na kocha (Gamondi), anaendelea kufanya maandalizi ya mechi yetu hiyo kwa sababu haijaisha hadi iwe mwisho, Al-Merrikh ina wachezaji wazuri na tunatakiwa kujipanga vizuri kwa kuwa haitakuwa rahisi," alisema meneja huyo.

Naye Daktari wa Yanga, Mosses Etutu, alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri akiwamo Joyce Lomalisa aliyeumia nyama za paja kwenye mechi dhidi ya Namungo FC na tayari anaendelea na mazoezi.

"Halikuwa jeraha kubwa, alipata matibabu na kupumzika kwa siku chache na tupo imara, amejiunga na wenzake katika mazoezi ya kuchezea mpira," alisema Etutu.

Wakati huo huo Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema Al-Merrikh wanatarajia kutua leo saa 9:00 alasiri kwa mchezo huo ambao wameupa jina la 'Ki Day', kwa ajili ya kiungo wao, Stephane Aziz Ki.

e

ncalo
si ya
kisha
sti ya
wa
nabao
klabu
gazia
kwa
ubwa
nina
maye
afura-
kesho
zima
nata."

# Michezo

Jumatano Septemba 27, 2023

Nipashe




## Enrique aondoa hofu kwa Mbappe

UKURASA 22



# TWIGA STARS YASONGA MBELE WAFCON

Wachezaji wa Twiga Stars wakishangilia baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ivory Coast katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana na kisha kuitupa nje kwa mikwaju ya penalti 4-2 kutokana na matokeo ya jumla kuwa mabao 2-2. Mechi hiyo ilikuwa ya kuwania kufuzu WAFCON mwakani. **Habari Ukurasa 20. MPIGAPICHA WETU**

## Inonga kurejea wiki ijayo

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikitangaza rasmi kuwa beki wake wa kati, Henock Inonga, anatarajia kurejea dimbani mapema zaidi ya ilivyodhaniwa wiki ijayo, kikosi cha Simba jana kilipata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Pan African katika mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam.

Daktari wa klabu hiyo, Edwin Kagabo, amethibitisha jana kuwa beki huyo atarejea wiki ijayo kwani maendeleo ya jeraha lake ni mazuri, akisema hakuumia sana kama watu wengi walivyodhani.

"Mpira wa miguu ni wa kugusana, nadhani baada ya wachezaji wenzake kufika pale na kuona damu nyingi iliyokuwa inatoka kwenye jeraha walionekana kushtuka sana na ndiyo iliwapa picha mashabiki jukwaani na waliokuwa wanatazama kwenye televisheni kuona kama ameumia sana au amevunjika.

"Kilikuwa kidonda chenye sentimeta 10 kwa nne, urefu na upana, matibabu yake ni kwamba alishonwa nyuzi 13, lakini kila kitu kwenye matibabu kilikwenda vizuri," alisema daktari huyo.

Alisema itamchukua Inonga wiki moja na nusu kupona na kuanza mazoezi, lakini siku hizo zinahesabika tangu alipoumia.

Simba ilicheza dhidi ya Coastal Union Alhamisi iliyopita Uwanja wa Uhuru na kushinda mabao 3-0 na kwa mujibu wa daktari huyo siku hizo zinahesabika tangu alipoumia, hivyo ina maana wiki ijayo ataanza mazoezi na wenzake.

"Kidonda chake kilikuwa kwenye mguu wake wa kulia hali yake kwa ufupi inaendelea vizuri, sasa hivi tunadili zaidi na kuuguza jereha lake na kwa hali ilivyo inaashiria uponaji wake utakuwa mzuri na wa haraka zaidi, kwa sasa tunahakikisha tunaweka dawa, kukifunga na kukifungua pamoja na matibabu mengine kama vile kumpa anywe dawa za kuua bakteria na za kutuliza maumivu, pengine Mungu akipenda ndani ya wiki moja na nusu tangu alipoumia atakuwa tayari kurejea kwenye uwanja wa mazoezi," alisema Kagabo.

Kuhusu majeruhi mwingine, Aubin Kramo, alisema bado anaendelea na mazoezi na siku si nyingi watawatangazia wanachama na mashabiki wa Simba ni lini na yeye atarejea uwanjani.

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi kuishangaza Al Merrikh

**Na Saada Akida**

● ● ● Ni wakati wakitua leo mchana, asema wataivaa kivingine kabisa huku akitaka...

KATIKA kuhakikisha anawapoteza maboya kabisa wapinzani wao Al-Merrikh kwenye mechi ya marudiano Jumamosi wiki hii, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amebadili mbinu kwenye kikosi chake lengo likiwa ni kupata matokeo chanya na kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga ambayo mchezo wa awali nchini Rwanda iliibuka na ushindi wa mabao 2-0, Jumamosi itaikaribisha Al-Merrikh katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, majira ya saa 1:00 usiku, ikihitaji sare yoyote ama ushindi ili kutinga hatua ya makundi kwa mara ya kwanza baada ya miaka 24.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Gamondi alisema anaamini mbinu alizobadilisha zitawavuruga wapinzani wao hao, ambao watakuja wakijua watacheza kama walivyofanya katika mechi ya kwanza.**

Alisema baada ya kumalizika kwa mchezo wa ligi dhidi ya Namungo FC, wamerudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi changamoto zilizoonekana na kuongeza na kutoa programu maalum kwa ajili ya kuwa imara zaidi wawapo uwanjani.

"Kila mchezaji ana jukumu la kupambania nembo ya timu, wote nimewapa mbinu, kuwa imara kwenye mechi zote za ushindani ikiwamo dhidi ya Al Merrikh, wachezaji wanatakiwa kusahau matokeo ya nyuma.

"Tumeshinda mechi ya kwanza haina maana wapinzani wetu ni wabaya, hakuna bali tuliwazidi sehemu, natarajia watabadilika kwenye mechi yetu, tunatakiwa kubadilika kwa ajili ya kupata matokea mazuri zaidi," alisema kocha huyo.

Alisisitiza kwa sasa washambuliaji wamekuwa wakifanyia kazi mbinu alizowapa hasa kwenye nafasi wanazotengeneza kuzigeuza kuwa mabao, pamoja na mabeki kuwachunga wachezaji hatari kutoleta madhara langoni mwao.

"Tuna washambuliaji na wachezaji wenye uwezo mkubwa na kila mchezaji tayari anajua mbinu kwa ajili ya kuwa imara zaidi kuelekea mechi ya Jumamosi kuwania kufuzu kucheza makundi," alisema kocha huyo raia wa Argentina anayetamani kuifikisha Yanga makundi.

Aliongeza kuwa ushirikiano uliopo kwenye benchi la ufundi pamoja na nguvu za wachezaji kutimiza majukumu yao unaongeza kasi ya kufikia mafanikio ambayo wanayatarajia.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >